

SISI TUNATAKA KUMWONA YESU



Asante, Ndugu Borders.

² Mnaweza kuketi. Hakika ninayahesabu haya kuwa ni majaliwa makuu kuwa hapa, usiku wa leo. Na sijui kama ninaweza kutamka hilo jina vizuri, Santa Maria, nadhani hivyo ndivyo mnavyolitamka. Na ndiyo fursa yangu ya kwanza kuwa hapa katika jiji hili la kupendeza, na kufurahia mazingira ya ushirika mzuri na hali nzuri ya hewa.

³ Tulipitia Phoenix hivi majuzi wakati ilikuwa yapata mia moja na kumi na moja, tulipofika huku juu, mbona, nilikuwa karibu tayari kutafuta kabuti langu. Je, hiyo . . . hii ndiyo hali ya hewa mwaka mzima, karibu hivi? Mtu fulani alisema ilikuwa hivi karibu wakati wote. Hamna nyumba tupu karibu na hapa, siyo, ambayo mngetaka kupangisha kwa muda? Hapa ni mahali pa—pazuri sana pa kuishi, penye hali hii ya hewa ya namna hii hapa. Mimi . . .

⁴ Mtu fulani alikuwa akiniambia mkahawani, leo, kasema, “Mbona, wakati wetu wenye joto sana wa mwaka ni karibu Desemba!” Kasema walikuwa wakichoma nyama huko nje uani kwa ajili ya Krismasi. Sasa, kama ungalitoka nchini mwangu, uhomee nyama uani, ungevaa kabuti, na pamba ya masikio, na kuketi kwenye kipande cha barafu mahali fulani ku—kuchoma nyama.

⁵ Ni vema kwamba Mungu ameitengeneza dunia hii hivi kwamba sote tunaweza kuwa na furaha, kama tu tungejaribu kuwa hivyo, kuishi kwa furaha, na—na kumshukuru kwa yale tuliyo nayo. Nina hakika kabisa ya kwamba moja ya makosa yetu makuu, ni kwamba hatuna shukrani vya kutosha kwa yale tuliyo nayo. Amekuwa mwema sana kwetu kutupa vitu vingi vizuri, wala—wala sisi—sisi hatuonekani kuvithamini jinsi tunavyopaswa.

⁶ Nimekuwa na fursa, kusafiri sana, kote ulimwenguni mara kadhaa, na—na kuona mataifa mengine na watu na jinsi wa—jinsi inavyowalazimu kuishi na kadhalika. Kuna msemu wa kale, “Ni jambo kuu kuwa Mmarekani.” Vema, hiyo ni zaidi kidogo tu ya msemu, hiyo ni kweli, hiyo ni kweli kabisa, naam, ambapo tunaweza kupata chakula kingi, na—na kutulia, na maskini shida zetu ni ndogo, na karibu tunaishi katika ule Utawala wa Miaka Elfu. Kama tukiini . . . tukiondoa tu dhambi ninaamini ingekuwa ni ule Utawala wa Miaka Elfu basi.

⁷ Lakini tuna furaha, hata hivyo, kuwa na taifa hili. Hatujui ni muda gani zaidi tutaweza kuwa nayo hivi, bali tunatumaini ya kwamba itakuwa hivyo mpaka Bwana Yesu atakapokuja. Huu ndio mshiko wetu mkuu wa mwisho wa ustaarabu, tunaamini, na kuona mataifa mengine, jinsi yalivyoinuka na kuanguka, nasi tunaona letu likipitia njia ile ile, kwa hiyo tu—tunahuzunika kwa sababu ya hilo. Lakini hata hivyo, tunajua ya kwamba hilo linanena tu ya kwamba tuna Mji, na Taifa ambalo halitaangamia kamwe.

⁸ Si muda mrefu uliopita nilienda kwenye mti nilikokuwa nikienda nilipokuwa mvulana mdogo, nao ulikuwa ni mti mkubwa mzuri sana. U—ulikuwa ule tunaouita mashariki kule, mashariki ya kati, mfue. Nayo ni mti wenye maisha marefu, na unapendeza sana na ni wa kipekee, ambapo haisongwi na miti mingine, na imeumbika vema. Nami nikawazia, “Mti huo utasimama kwa vizazi kadhaa.” Lakini mwajua, ni kisiki tu sasa, nami nakumbuka ku- . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . nilipokuwa na umri wa miaka saba au minane, kulikuwa na chemchemi chini yake, nilikuwa nikienda kuinywea chemchemi hiyo. Hiyo chemchemi hata imekauka, huo mti haupo tena.

⁹ Ninakumbuka maskini ile nyumba tulimokuwa tukiishi, ilikuwa ni nyumba ya magogo. Tulikuwa na ninii ndogo. . . Mama alikuwa na kipande cha kioo cha kujitazama, kioo alichokuwa amekining'iniza juu ya mti huko nje ambako tulikuwa na benchi ndogo ya kunawia, nasi tungekuja kutoka kondeni na kunawa, na—na tulikuwa na gunia kuukuu la unga ambalo Mama alikuwa amelifanya taulo. Sijui kama ninyi watu mlipata kuishi namna hiyo ama la, lakini sisi Wakentaki tulikuwa na wakati mgumu sana.

¹⁰ Kwa hiyo basi ninakumbuka alikuwa akivuta nyuzi kutoka chini yake na kufanya vitu kama pindo ndogo, na kuining'iniza chini. Nayo taulo hiyo iliyoparuza, na wakati sisi watoto tulipooga nayo, whiu, na inabidi tusuguliwe, karibu ingetoa ngozi.

¹¹ Na—nami nilikuwa nikimwona baba yangu, mtu mdogo wa kimo, ingawa mwenye nguvu, alikuwa mkata miti. Naye angevuta, aingie, akunje mikono ya shati lake wakati anapoenda kuoga, alikuwa wakati huo, nadhani, katika miaka yake ya ishirini na kitu, ishirini na mitano, umri wa miaka thelathini, naye alikuwa na misuli mikubwa mno, na yenye nguvu. Nilisikia mtu akiniambia, ilikuwa ni mwaka jana, mwanamume, alikuwa akitufanyia kazi, alisema alimwona akipakia gogo-majivu lenye uzito wa ratili mia tisa peke yake. Ndipo nikawaza, “Mkono wa mtu yule!” Nikasema, “Jamani, ataishi miaka mia moja na hamsini!” Lakini mwajua, alikufa akiwa na umri wa miaka hamsini na miwili.

Inaonyesha tu ya kwamba, “Hapa hatuna mji udumuo, bali

tunautafuta Ule ujao.” Hiyo ni kweli. Tunautafuta Mmoja ambao utadumu milele.

¹² Na sasa, marafiki Wakristo, hii ikiwa ndiyo mara yangu ya kwanza miongoni mweni hapa katika—katika mji wenu... Nami ninayahesabu kuwa ni majaliwa makubwa kwamba wachungaji wenu wamenialika kuja. Nami nipo hapa kufanya yote niwezayo kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Wala mimi si mhubiri sana, mimi ni...bali ninampenda Bwana. Kama mhubiri mzuri anampenda kuliko ninavyompenda, pamoja na ujinga wangu, nashangaa tu jinsi wanavyoendelea nao, ku—kuuvumilia tu, kwa sababu wakati mwingine ninaninii, ninampenda sa—sana moyoni mwangu, ni vigumu kwangu kutulia.

¹³ Na hili si jambo fulani tangu nilipoanza kuzeeka, nilianza hili nilipokuwa mvulana tu, mvulana mdogo tu, nilimpa Bwana Yesu maisha yangu na kumtumikia tangu wakati huo. Nayo... kila siku, kama ninavyojua ninakaribia ufuko wa Ng’ambo ya pili, inazidi kuwa tamu kila siku. Ninampenda tu kadiri miaka inavyopita.

¹⁴ Nami nimekuja kuweka ushirika wangu na... pamoja nanyi ndugu na dada, ndipo sote tuvute kwa ajili ya Ufalme wa Mungu, tupate baraka za Mungu, ndipo niulete huu Ujumbe mdogo ambao Bwana amenipa kwa ajili yenu, na kuusikia ujumbe wenu ambao Mungu amewapa tena kwa ajili yangu. Nasi tutawaombea wagonjwa, ndipo tuone kama kuna mtu yeyote anayetaka kujiunga na jeshi hili kuu, sio dhehebu, ushirika tu pamoja na Kristo. Mnaona? Hatuwakilishi dhehebu lolote, tunawapenda wote, hakuna lolote dhidi yao, ila kwetu sisi, tunasimama tu tukiwa huru.

¹⁵ Na, kama nilivyosema hivi majuzi, tuko hapa tukivua samaki pamoja. Sasa, ninii... Yesu alisema, “Ufalme wa Mungu umefanana na mtu aliyechukua jarife, na kulitupa baharini, na akisha kuvuta huo wavu, akauchukua huo wavu, alikuwa na wa kila aina.” Bila shaka alikuwa na samaki wazuri, na samaki mla mizoga, na kamba, na kasa, na nyoka, na vyura, na kila kitu kilicho majini, lakini hao ndio wanaoshikwa na uamsho. Mnaona? Hiyo ni kweli.

¹⁶ Kwa hiyo ndugu zetu, hapa, wamekuwa wakivulia kwenye kona yao na huko chini kwenye kona ya pili wakivua, na sasa nimekuja kuunganisha *wavu* wangu na zao ili tuweze kufikia mbali huku, kote mjini, na kuvuta kwa kila kitu tuwezacho. Na hilo ndilo lililotuleta hapa, kuungana pamoja tuone... hatuwezi kamwe kumudu kuninii...lakini yale, baada ya kujua yale tunayojua kumhusu Kristo, ni kufanya kila jitihada tuwezayo. Hatutaki mtu yeyote akose Mahali hapo patukufu ambapo ameenda kuandaa. [Ndugu Branham anakohoa—Mh.] (Samahani.) Nasi tuko hapa kusaidia. Sasa, nitajaribu na...

17 Wanasema ya kwamba hakujakuwako na yeyote wa hao ndugu, sidhani, hapa, wa wale wainjilisti wakubwa, kama vile Ndugu Billy Graham, Oral Roberts, na hao wainjilisti mashuhuri. Basi, mimi... Ambalo, labda baadhi yenu mmewasikia. Nami na—nadhani, kwa kuwa ni mji mdogo, na hapana budi kuwe na kiasi kikubwa cha fedha kinachohusishwa na mkutano mkubwa kama huo. Nami nakisia fedha za Ndugu Roberts kila siku ni zaidi ya dola elfu kumi, kumi na mbili kwa siku kwa ajili ya televisheni yake, radio, na kadhalika. Nami nadhani Billy Graham hutumia hizo au labda zaidi. Sasa, watu hao wangewezaje kufika mahali padogo kama hapa? Wa—wasingeweza kufanya hivyo. Mnaona?

18 Lakini wakati Bwana aliponiita, Yeye... Mwajua, kamwe si—sikuanzisha radio yoyote, ama—ama televisheni, ama chochote kile ili niwe, mwajua, nifungwe kabisa, hivi kwamba ningeweza kwenda popote Bwana aliponiita, maana sihitaji pesa. Kwa hiyo mimi huninii tu—kamwe sina miradi ya kudhamini, hata kidogo, na kuenda tu na kushirikiana na watu, na kokote Bwana angeniita niende. Nami nina... Yeye ana... nilikuwa na majaliwa makuu.

19 Nilihubiria, hivi majuzi tu, uamsho wa siku mbili usiku katika kanisa lililoenea watu ishirini, kisha nilikuwa huko Bombay, India, ambako tulikuwa na laki tano kwenye mkutano mmoja, na Durban, Afrika Kusini, kama laki mbili na ishirini na tano elfu, ambako niliona makafiri kabisa elfu thelathini wakimkubali Kristo kama Mwokozi katika wito mmoja wa madhabahuni.

20 Kisha nikawaona wameokota yapata malori saba makubwa, na hayo malori, jamani, *hilo* lingekuwa ni Jeep ukilinganisha na hayo magari makubwa ya Kiafrika kule, ya viti vya magurudumu vitupu, mikongojo, na kadhalika wenyeji walivyokuwa wamebebania, huko chini kutoka mi—misituni.

21 Ndipo kesho yake asubuhi wakati Sidney Smith, meya wa—wa Durban, Afrika Kusini, aliponipigia simu na kusema, “Nenda dirishani ukaangalie kuelekea ufuko wa bahari.” Na hapa ukaja msururu wa watu wenye... ambapo miujiza ishirini na tano elfu ilikuwa imefanywa kwa ombi moja, nao hao hapo na magongo yao na viti vyao vya magurudumu. Nao wenyeji, ambao walikuwa na vita juma moja kabla, walikuwa wakitembea, walikuwa wamelala kwenye magongo hayo, na magango, na kadhalika, kesho yake wakitembea kwa amani, wamekumbatiana, wakiimba “Mambo yote yanawezekana, amini tu,” katika lugha yao ya kienyeji.

22 Hivyo ndivyo ulimwengu mzima unavyopaswa kuwa ukifanya, usiku wa leo...?... sisi sote kwa moyo mmoja na nia moja, tukiimba tu Injili tukufu ya Bwana Yesu.

²³ Na sasa, katika ujumbe nilio nao, nitajaribu kuufanya rahisi tu iwezekanavyo, kwa sababu kwa kuwa ndiyo mara ya kwanza ambayo... labda watu wamekuwa mikutanoni, na huenda likaonekana ni jambo geni kwenu kwanza, na kama ndivyo, ninawaomba tu kama mtanivumilia kidogo, mnaona, na sikuzote mchunguze yale ninayosema, na kama hayaambatani kabisa na Maandiko, msiyaamini, mnaona, maana...

²⁴ Sasa, Mungu anaweza kufanya mambo ambayo hayajaandikwa katika Biblia, Yeye ni Mungu, anaweza kufanya chochote atakacho. Mnaona? Lakini mradi tu ninamwona akifanya yale hasa aliyohidi kufanya, hilo litakuwa sawa vya kutosha kwangu, hilo ni kweli. Ndipo ninajua niko kwenye njia sahihi, basi, mradi tu yako katika Maandiko, Mungu aliahidi kufanya hivyo. Na jinsi alivyolifanya, na jinsi anavyolifanya, nami ninaamini... Hivi ndivyo ninavyoamini: kwamba kama Yeye aliwahi kuwa Mungu, Yeye angali ni Mungu. Mnaona? Na kama Yeye si Mungu yeye yule aliyekuwa, basi Yeye hakuwa Mungu, mnaona, kwa sababu Yeye ni... iwapo Yeye ni Mungu, hana budi kuwa asiye na kikomo, asiye na kikomo, na halafu, kama Yeye hana kikomo, Yeye ni mkamilifu.

²⁵ Na kama Mungu akiwahi kufanya jambo lolote, mnaona, kama Yeye... kumbukeni tu sasa, kama Mungu akiwahi kufanya jambo lolote, na jinsi anavyolifanya, kamwe hawezi kubadilika hivyo, kwa sababu, unaona, Yeye ni mkamilifu. Sasa, ninaweza kufanya jambo fulani, nawe unaweza kufanya jambo fulani, na mwaka ujao tu—tuna wazo bora zaidi, mnaona, kwa sababu tulijifunza zaidi kidogo, na labda katika miaka kumi sisi ni werevu zaidi kuliko tulivyokuwa, bali si Mungu, Yeye hana kikomo. Mnaona? Kwanza kabisa Yeye ni mkamilifu.

²⁶ Na—na kama Mungu akipata kuitwa kufanya uamuzi, basi uamuzi anaofanya hauna budi kubaki hivyo milele, hawezi kuufanya *hivi* wakati mmoja, na mwingine *hivi*, achukue *hili* na kukataa *lile*, jinsi anavyotenda mara ya kwanza, kama hatendi hivyo kila wakati, alitenda vibaya mara ya kwanza, mnaona, kwa sababu Yeye ni Mungu. Kamwe hawezi kubadilisha njia Yake, maana Yeye ni Mungu. Halafu basi, Yeye hana kikomo, yuko kila mahali, ana nguvu zote, na kusudi awe Mungu hana budi kuwa vitu hivyo vyote, kwa hiyo tunaamini hivyo.

²⁷ Na sasa, nami nitajaribu, katika kuyaelezea Maandiko, na kusoma, na kila kitu, kulifanya rahisi tu nijuavyo ku—kulifanya. Halafu basi, sasa, na kulifuatilia kwa makini katika Maandiko. Na kisha nitawaomba mniunge mkono kwa maombi, kwa sababu...

²⁸ Na si lingekuwa ni jambo zuri sana kama kungekuwako, mumu humu katika mji huu mdogo wa Santa Maria, uamsho mkuu ukitokea katika makanisa yote? Ingekuwa... na watu wangekuwa wakimiminika kupitia milima hii, kutoka huko

chini kupitia vilimani, wakija kuona utukufu wa Mungu, na makanisa yote yakiwaka tu moto kwa ajili ya Mungu, na—na zile tofauti ndogondogo zikaondolewa, na kila mtu, moyo mmoja na nia moja. Mbona, lingekuwa ni jambo zuri sana! Wazia tu, maskini Santa Maria, huko karibu na pwani ya ziwa, kungekuwa ndiko . . . kulikokuwa na uamsho huu.

²⁹ Sasa, si—si kwamba tu huenda ikawa, bali inawezekana kwamba ingetukia, inategemea mtazamo tunaochukua. Sasa, Mungu daima hutuma karama Zake na kadhalika katika vizazi, katika makanisa, na msimamo wowote ambao watu wanachukua, hayo ndiyo matokeo ya kile wanachopata, tunajua hilo. Wewe . . . Mungu hajisukumizi kwa mtu yeyote, huna budi kumtaka.

³⁰ Sasa, hakuna mtu anayeweza kumwelezea Mungu. Inakubidi kumkubali Mungu kwa imani, kwa sababu kama si imani, basi si Mungu. Kama ningeweza kumwelezea Mungu, basi ningekuwa sawa na Yeye. Na sasa, hatuwezi kufanya hivyo, hatujaribu kufanya hivyo. Lakini vitu vidogo ambavyo ametupa, tunachukua tu ahadi Yake, na kuiamini, na kuiangalia ikitendeka kazi jinsi hasa Yeye alivyosema ingefanya; na kama tutafanya hivyo, nina hakika tutauona utukufu wa Mungu.

³¹ Sasa, sitaki kuwaweka muda mrefu sana usiku. Ili tu . . . Ninajua ninyi ni watu wanaofanya kazi, na—nami nimefanya kazi maishani mwangu mwote, kwa hiyo ni—ninajua ilivyo kulazimika kwenda nyumbani, na kuamka mapema asubuhi, na, baada ya kuketi kwenye mkutano. Nami nimekuwa na ya muda mrefu sana, kwa hiyo . . . lakini tutajaribu kumalizia kila usiku, tuseme . . .

³² Sasa, bado dakika ishirini ifike saa tatu, kufikia wakati huu, nami nadhani labda ibada yenu kwa kawaida humalizika yapata saa tatu na nusu, na hiyo itawapa wakati wa kwenda nyumbani na—na kupumzika, na kurudi kesho usiku. Chukueni simu, na kumpigia mtu fulani, mkawaleta wagonjwa na wanaoteseka. Wala msi—msiingie kana kwamba mlikuwa tu . . . kuingia tu haraka namna hii, na kurudi upesi, mnaikosa maili mia moja, mnaona. Mnaona?

³³ Kama ingekubidi kwenda kwa Mayo Brothers, unajua, kwa uchunguzi wapate kujua shida yako, jambo la kwanza, ingekubidi kupiga simu na kupata miadi. Na hiyo labda ingekuchukua miezi miwili au mitatu kabla ya kupata miadi. Halafu basi utaenda kule na kukaa hospitalini, labda kwa juma moja ama siku kumi hospitalini, wala hawakufanyii lolote ila kukuchunguza.

³⁴ Ndipo basi, ukimalizana na hayo yote, baada ya miezi kadhaa ukitoa jasho, na kuchunguzwa, na dawa, na, loo jamani, kila kitu, ndipo wanakwambia tu shida yako. Unaona? Hiyo ni kweli. Na hata hivyo, watu wanasongamana kutoka kila mahali

wapate kujua shida yao, wakati, kama tu utamwamini Mungu, kwa moyo wako wote, itakwisha katika dakika moja. Unaona? Kama ukininii tu. . . Unaona? Hiyo ni kweli. Na ni. . . Huna budi kuliadini hata hivyo. Na sasa kumbukeni, ni kwa imani tu, tunaliadini na kuliona likitenda kazi.

³⁵ Halafu basi, kila usiku Maandiko ninayotumia, wakati mwingine ninaandika Maandiko kadhaa hapa ya kurejea, na kama nikiyarejea Maandiko haya, na yale mnayoona yakitukia, kama hayaonekani ya kawaida kwenu, nenda nyumbani ukayachunguze kwa Biblia. Basi mnawajibika kwangu, kama si ahadi ya Mungu, kurudi na kuniambia habari zake, na kuyaweka hapa juu ya dawati langu na kusema, “Ndugu Branham, hilo si sawa, hilo si Maandiko.” Mnaona? Na kama ni—ni Maandiko, basi ni, basi ni juu yako kuliadini, sivyo? kwa—kwa kuwa ni Mungu.

³⁶ Sasa, kabla hatujachukua muda mwingi sana sasa, basi ninataka kuwashukuru ndugu zangu tena, nadhani hawa ni wahudumu, na kadhalika, hapa, ninathamini hilo, nanyi washiriki, na washi-. . . washiriki wa sehemu mbalimbali za huu mwili sisi ni wageni hapa, sisi ni wasafiri, nasi tunakuja kuwatembelea ninyi mnaosafiri. Tunakungojea kuja kwa Bwana. Hapa hatuna mji udumuo, tunaenda mahali mahali, na kungojea kule kuja kwa Bwana. Siku baada ya siku tunazeeka zaidi na zaidi, wala hatujui ni dakika gani, kama sisi ni vijana au wazee, ambapo uhai wetu [Ndugu Branham anadata vidole vyake—Mh.] unaweza kunyakuliwa namna *hiyo*. Ndipo hatuna budi kukutana na Mungu, na hapo. . . Huu ni wakati wetu wa maandalizi, kwa hiyo hebu na tujiandae sasa kumlaki Bwana atakapokuja.

³⁷ Sasa, hebu na tuinamishe vichwa vyetu na kuzungumza na Mwandishi kabla hatujasoma Neno Lake. Sasa, huku vichwa vyetu vimeinamishwa, na mioyo yetu vile vile, nashangaa, humu jengoni usiku wa leo, kabla hatujaanza, kama kungekuwako na wale hapa ambao wangetaka tu kumwinulia Mungu mkono wao na kusema, “Mungu, sasa katika mkutano huu nina haja. Je, utanipa haja yangu, Bwana? Nitainua mkono wangu na kwa hii tu. . .” Mungu awabariki, kila mahali. Sasa, Yeye anaona kilicho chini ya mkono wako moyoni mwako.

³⁸ Baba yetu wa Mbinguni, sasa tunakikaribia Kiti cha Enzi cha neema Yako. Sasa, tusingekuja kwenye Kiti cha Enzi cha haki, kwa sababu kama tungelipata haki sote tungekuwa. Tusingeweza kuja kwenye Kiti cha Enzi cha Hukumu, bali tumealikwa kuja kwenye Kiti cha Enzi cha neema, pamoja na ahadi ambayo Bwana wetu alitwambia, “Mkimwomba Baba lolote katika Jina Langu, nitaninii. . . mtapewa.” Sasa, tunajua ya kwamba hiyo ni kweli, haina budi kuwa ni kweli, ni Neno. Nasi tunaadini Biblia hii kuwa ni Neno Lako lililokosea, kila

Neno Lake ni la Mungu, nasi tunalishikilia na kulithamini kwa mioyo yetu yote.

³⁹ Wewe unajua jinsi tunavyouthamini wakati huu wa ushirika hapa, katika mji huu mdogo wa kupendeza, na hawa ndugu na dada wazuri. Tunakumbushwa juu ya siku ya mwanzoni wakati mitume walipokutana pamoja wakati idadi yao ilipokuwa ndogo, lakini jinsi Roho Mtakatifu alivyokuja miongoni mwao na kufanya mambo makuu mno, kwa sababu Kanisa lilikuwa limekusanyika pamoja! Hilo lilikuwa ni Kanisa katoliki la kimitume la mwanzoni, huko nyuma kabisa tangu mwanzo, kwenye Pentekoste.

⁴⁰ Tunaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba, wakati Kanisa hili la katoliki ya kimitume limekusanyika pamoja ya kwamba utarudi, usiku wa leo, katika umbo la Roho Mtakatifu, miaka elfu mbili tangu kusulubiwa Kwako kwa ajili ya ukombozi wetu, kafara ya ninii yetu... kwa ajili ya uovu wetu, ukitoa maji ya farakano kwa kuoshwa kwa maji kwa Neno, na sasa, kulifanya Neno Lako hai, kulihuisha na kulitimiza. Inahitaji Mungu aliye hai, aliyefufuka apate kufanya hivyo.

⁴¹ Na sasa, Baba wa Mbinguni, tungeomba, usiku wa leo, ya kwamba Uwepo Wako ungekuwa mkuu sana miongoni mwetu, hata tutakapoondoka humu jengoni, usiku wa leo, kusanyiko hili dogo, hata kwenye usiku wa kwanza, jalia tuseme kama wale, waliotoka Emau wakati huo baada ya ufufuo asubuhi hiyo. Ulikuwa umetembea nao siku nzima, ukazungumza nao, hata hivyo hawakukutambua; na, Baba, nina hakika baadhi yetu, na wengi wetu, na karibu sisi sote hapa tumetembea pamoja na Wewe, Nawe umetembea pamoja nasi, na hata hivyo hatukujua Hilo.

⁴² Lakini wakati wa jioni ulipofika, wakati taabu za mchana zilipokwisha, Wewe uliwakusanya pamoja, nayo milango ikafungwa, na ndipo ukafungiwa ndani pamoja nao, ndipo ukafanya jambo fulani kama tu ulivyofanya kabla ya kule kusulubiwa, nao wakatambua, kwa jinsi ulivyolifanya, ya kwamba Huyu alikuwa ni Wewe. Nao... Ndipo ukatoweka machoni pao, nao wakafanya hima kwenda nyumbani, kwa wenzao wengine na kusema, "Hakika, Bwana amefufuka."

⁴³ Hivi Wewe, usiku wa leo, Baba, kwa kuwa tumekusanyika pamoja na kufunga milango kutuzunguka, hivi Wewe hutajitokeza miongoni mwetu na kufanya jambo fulani, usiku wa leo, kama ulivyofanya ulipotembea Galilaya, na Kapernaumu, na sehemu mbalimbali za ulimwengu? kwamba kusanyiko hili dogo, na sisi sote pamoja, tuweze kuona thibitisho la ufufuo. Masihi mkuu wa Mungu yu hai, baada ya miaka elfu mbili kupitia kwa wakosoaji na mahali penye giza, lakini hata hivyo hawawezi kumwua tena, Yeye yu hai milele. Tujalie, Baba.

44 Basi tujalie, tunapoenda nyumbani usiku wa leo, tuseme, tukienda zetu, “Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, hapo alipokuwa akisema nasi njiani?” Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu, na kwa ajili Yake. Amina.

45 Sasa, katika Yohana Mtakatifu, mlango wa 12 na kifungu cha 20, tunasoma kwa ajili ya msingi kidogo kwa ajili ya muktadha:

Palikuwa na Wayunani kadha wa kadha miongoni mwa watu waliokwea kwenda kuabudu kwenye sikukuu.

Basi hao walimwendea Filipo, mtu wa Bethsaida ya Galilaya, wakamwambia, wakisema, Bwana, sisi tunataka kumwona Yesu.

46 Halafu katika Waebrania 13:8: [Ndugu Branham anakohoa—Mh.] (Samahani.)

Yesu Kristo yeye yule jana, . . . leo, na hata milele.

47 Sasa, hili ni somo kwelikweli. Na kwa ajili ya msingi kidogo, huenda tukasema kwamba hawa Wayunani walikuwa na udadisi ule ule nilio nao usiku wa leo, nami ningeamini sote tungekuwa nao. Hakuna mtu aliyewahi kusikia habari za Yesu pasipo kutamani kumwona. Kama ningeliambia maskini kusanyiko hili, usiku wa leo, “Ni wangapi wenu wangependa kumwona Yesu?” Nadhani kila mkono humu ndani ungeinuliwa. Hiyo ni kweli. Hebu tulijaribu tu. Ni wangapi wangetaka kumwona? Hebu tuone. Mnaona hapo? Hakika. Mmesikia habari Zake, “Imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno la Mungu.”

48 Sasa, sote tungependa kumwona Yeye, hakika. Ningependa kumwona. Vema, sasa, kama Yeye . . . Hilo lingetuweka mahali pale pale ambapo hao Wayunani walikuwa. Walimjia Yesu wakasema . . . waliwajia wanafunzi wakasema, “Bwana, Bwana, sisi tunataka kumwona Yesu. Sisi . . .” Hiyo ndiyo shauku yao, “Tunataka kumwona Yesu.” Ndipo Filipo akawachukua na—na kuwaleta kwa Yesu, yeye na mtume mwingine, nao wakapata kumwona Yesu.

49 Sasa, Waebrania 13:8 ilisema ya kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Na kama tunatamani kumwona, kwa nini hatuwezi kuwa na majaliwa yale yale waliyokuwa nayo? Sasa, mnaona, Maandiko hayawezi kusema uongo, Hayana budi kuwa ni ya kweli, mnaona, Hayana budi kuwa ni ya kweli. Sasa, kama Biblia ilisema Yeye ni yule yule, kwamba . . . Hana budi kuwa yeye yule. Sasa, siamini Biblia ni, ya kufasiriwa apendavyo mtu yeyote, ninaamini ni jinsi tu ilivyoandikwa.

50 Ninaamini ya kwamba itambidi Mungu kuwa na Kigezo fulani ambacho atauhukumu ulimwengu kwacho. Sasa, mimi, kama nyote mnajua, nikiwa Mwairishi, nilitoka kwenye msingi wa familia ya Kikatoliki. Na sasa, nilipokuwa mvulana

mdogo... Bila shaka, baba na mama yangu walifunga ndoa nje ya kanisa, na, nje ya kanisa Katoliki, na kwa hiyo, hawakuwa... hawakuwa wafuasi wa chochote. Nanyi mlisoma hadithi ya maisha yangu, labda. Kama hujaisoma, vitabu viko hapa, ndugu mmoja anavyo hapa kuviuza, na kadhalika.

⁵¹ Sasa, halafu katika jambo hilo, nilipopata wito kutoka kwa Mungu, nilianza kushangaa, sasa... Ndipo nilipoenda kanisani, kanisa linasema ya kwamba Mungu atauhukumu ulimwengu kwa kanisa. Vema, nikaja kugundua kuna yapata makanisa mia tisa mbalimbali. Na moja linasema wako sahihi, na hilo lingine limekosea; nao wako sahihi na hao wengine wamekosea. Sasa, kidogo linatatanisha namna hiyo. Sasa, kama la Lutheri liko sahihi, basi la Baptisti limekosea; kama la Baptisti ni sahihi, basi la Methodist limekosea. Na basi, yanatofautiana sana. Kwa hiyo basi katika hilo jambo lote niliona kulikuwako na mchafuko.

⁵² Mungu angewezeje kamwe kuruhusu... kisha awalete watu kwenye Hukumu iliyo kamili sana na halafu njia nyingi mbalimbali za kutokea? Mmoja *hivi*, na mwingine *vile*, mmoja anasema, “*Hii* ni sawa,” na huyo mwingine akisema, “La, siyo.” Na, “*Hii* ni ninii... njia *hii*, na *ile*...” Ingekuwa kidogo inatatiza. Nami ningeweza... sininii... singeweza kuamini ya kwamba Baba mwema wa Mbinguni angefanya jambo kama hilo.

⁵³ Kwa hiyo basi, nikawazia, “Vema, Yeye aliweka Hukumu juu ya watu kwa kitu gani mara ya kwanza? Yeye aliwapaje...?” Hiyo ilikuwa katika... kwenda, inabidi kurudi kwenye Mwanzo, kwa hiyo Mwanzo ndiyo sura ya mbegu, ambalo linamaanisha “mwanzo.”

⁵⁴ Basi jambo la kwanza ambalo Mungu aliweka mbele ya mwanadamu lilikuwa: Litii Neno Lake. Ndipo utelezi mmoja mdogo, si mlango mzima, mkubwa mno, bali kulielewa tu Neno vibaya, kuligeuza tu kidogo, Shetani alifanya hivyo, kwa kutoa hoja, nalo lilisababisha ninii yote... kila huzuni ya moyoni iliyopata kuwako, kila ugonjwa, kila mauti, kila mtoto mchanga mgonjwa, kila kaburi ubavuni mwa kilima, kutokuamini tu Neno moja dogo, kuninii tu, si kulitupilia nje kabisa, bali kulinukuu tu vibaya, hoja tu, “Hivi si ni jambo la busara kwamba Mungu asingefanya jambo kama hilo?” akasema. Lakini Mungu alisema angefanya hivyo. Mnaona?

⁵⁵ Halafu basi, kama Mungu akiachilia miaka hii yote elfu sita ya mateso, kwa sababu tu ya kuchukua Neno moja na—na kulipotosha, na kusababisha haya yote, Yeye atatuachaje turudi huku tukiwa na Neno lingine lililopotoshwa kabisa? Kwa hiyo tukiwa na madhehebu mia tisa na sitini na kitu mbalimbali, tunawezaje kuhukumu kwa hayo? Kila mtu akisema *hivi*, ama *vile*.

⁵⁶ Ndipo nikasoma katika hicho Kitabu ambapo, katika sehemu ya mwisho ya Kitabu cha Biblia, kilisema, “Yeye

atakayeondoa Lolote kutoka kwenye Kitabu hiki, ama kuongeza jambo moja Kwake, huyo ataondolewa kutoka kwenye sehemu yake ya Kitabu cha Uzima.” Hao ni makasisi, madhehebu, ama kadhalika, ambao—ambao wananukuu vibaya Neno, ama kuweka mafundisho ya sharti badala ya Maandiko, na kadhalika, na mawazo ya watu wenyewe kwa ajili ya mafanikio yao wenyewe. Halina budi kuwa ni Neno la Mungu hasa, jinsi hasa Yeye alivyolisema.

⁵⁷ Sasa, ninajua wengi wetu hatuna imani, nami sina, wana imani ya kufanya ahadi Zake zote kutukia. . . kutimia, lakini hakika nisingemzuia mtu aliyekuwa na imani ya namna hiyo. Kama ambavyo nimesema mara nyingi, “Laiti ningalikuwa na imani ya kutosha, kama aliyokuwa nayo Henoko, kufanya matembezi kidogo ya alasiri na kwenda Nyumbani pamoja Naye. Laiti ningalikuwa na imani ya namna hiyo.” Lakini mimi, endapo sina, sitamzuia mtu mwingine aliye nayo, nitasema, “Mungu ashukuriwe kwa ajili ya ndugu huyo wa thamani, dada ambaye ana imani ya kutembea moja kwa moja kutoka maishani bila ya kufa!” Na hilo lingekuwa zuri sana.

⁵⁸ Lakini tunaamini ya kwamba unakuja wakati ambapo kutakuwa na namna fulani ya matembezi ya alasiri ama asubuhi, na kutakuwako na wengi duniani, watakaonyakuliwa katika kule Kuja kwa Bwana. Nami naamini tunakaribia wakati huo.

⁵⁹ Sasa, sasa, Biblia inasema ya kwamba Yeye ni yule yule, hilo ndilo ninalojaribu kuwaelezea, kwamba hamna budi kutambua jambo hili: ya kwamba Biblia ilisema, “Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele.” Nao Wayunani walitaka kumwona, nao wakapelekwa Kwake na mmoja wa wanafunzi Wake. Basi, si ingewezekana, kama Yeye ni yeye yule, kwa mwanafunzi mwingine wa kweli kukupeleka Kwake, aache tumwone Yeye?

⁶⁰ Sasa, kimekuwa ndicho kilio cha moyo wa mwanadamu, tangu mwanzo wa wakati, kumwona Mungu. Ayubu, kile Kitabu cha kale kuliko vyote katika Biblia, wanadai kiliandikwa kabla ya Musa kuandika Mwanzo, sasa, kwamba Mus- . . . , ama, Ayubu alilia, “Loo, laiti ningalijua,” kwa maneno mengine “kujua mahali anapoishi, laiti ningaliweza kubisha mlangoni, laiti ningaliweza kuzungumza Naye!” Mnaona? “Laiti ningaliweza kuona mahali fulani ambapo ningeweza kwenda kubisha mlangoni! Ningependa kuhojiana Naye.”

⁶¹ Kila mtu anajaribu kuangalia nyuma ya pazia hilo, anajua ya kwamba alitoka mahali fulani kutoka gizani, anajua ya kwamba yeye yuko hapa katika maisha ya kibinadamu, naye anavuka pale tena mahali fulani. Kwa hiyo kila mtu anajaribu kujua mlango ni upi, na jinsi ya . . . mahali tulikotoka, na mahali tunakoelekea. Daima kimekuwa ndicho kilio cha moyo wa mwanadamu.

⁶² Na hata hivyo, kama tundesimama kwa muda kidogo tu, Yeye ni halisi sana karibu nasi mpaka kuna . . . Mbona, Yeye yuko tu kila mahali! Mungu ni . . . Yeye anaishi katika kila kiumbe kilicho na uhai ndani yake, anaishi mle; kila mmea, kila ua, chochote kile, Mungu anaishi ndani yake.

⁶³ Lakini sasa, badala ya kuingilia hilo, ambalo huenda tukafanya baadaye, ninataka kuwaletea jambo hili. Sasa, kama Yesu alikuwa katika Santa—Santa Maria usiku wa leo, ungemtafuta Mtu wa aina gani? Sasa, tunajua ya kwamba mwili Wake wa kawaida, ambao ulizaliwa na bikira Mariamu, uliosulubiwa, kisha ukafa, ukazikwa, na ukafufuka siku ya tatu, na kupaa juu kwenye mkono wa kuume wa Ukuu huko juu, umeketi pale, usiku wa leo, Kuhani Mkuu, anayeishi daima apate kutuombea tunapokiri. Naye pia ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu, sasa hivi Yeye ni Kuhani Mkuu wa namna hiyo anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu.

Sasa, njia pekee . . . Kama ningewauliza ninyi nyote Walutheri, “Mnaonaje juu Yake?”

“Mbona, Yeye angekuwa Mlutheri!”

“Wakatoliki wote?”

“Angekuwa Mkatoliki.”

“Mpentekoste?”

“Angekuwa ni Mpentekoste,” na kadhalika.

⁶⁴ Hebu tuninii tu . . . Njia pekee ya kweli ya kujua jambo hilo ni hii: Hebu tuone kile alichokuwa jana, na kama unaweza kuona kile alichokuwa jana, basi hana budi kuwa yeye yule leo, na atakuwa hivyo milele. Wekeni tu mwili wa kanisa kando, juu ya mawazo yao juu yake, na hebu tuone tu kile alichokuwa jana.

⁶⁵ Sasa, tunakumbuka ya kwamba Yeye ameahidiwa tangu bustani ya Edeni, tangu siku ya kwanza kabisa ya dhambi, ilipoingia katika bustani ya Edeni, ndipo Mungu akawaita Adamu na Hawa Hukumuni, Yeye aliahidi Uzao wa mwanamke unapaswa kukiponda kichwa cha nyoka, Mwokozi.

⁶⁶ Hatua nyingine kuu, tunamwona Musa, yule mkuu, vema, yeye alikuwa m—mfano wa Kristo, mtoa sheria, kuhani, mfalme, na kadhalika. Tunaona ya kwamba yeye alikuwa ni mfano mkamilifu wa Kristo, aliyezaliwa wakati wa mateso ya adui, akafichwa kwenye manyasi, na kama tu Kristo alivyofichwa, kisha akatoka, na kuwaongoza hao wana kutoka, na kadhalika. Na kwa hiyo tunaona pale ya kwamba Musa kwenye . . . huko karibu na mwisho wa safari yake, alisema sasa, baada ya kuondoka kwake kwamba “Bwana Mungu wenu atawaondokeshea Nabii, kama nilivyo mimi.”

⁶⁷ Sasa, tunajua ya kwamba Israeli yote, Agano lote la Kale, daima waliwategemea manabii wao. Waebrania 1 ilisema,

“Mungu, zamani alisema na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi, bali katika siku hii ya mwisho kupitia Mwanawe, Kristo Yesu.” Mnaona?

⁶⁸ Sasa, Waebrania, jinsi wangeweza kujua hilo... tumefundishwa katika Kumbukumbu la Torati, yapata mlango wa 18, “Akiwepo mmoja miongoni mwenu aliye wa kiroho au nabii, Mimi Bwana Mungu, nitajitambulisha Mwenyewe kwake katika maono, na kusema naye katika ndoto. Na kama yale nabii huyu asemayo yakitimia, basi msikieni. Lakini yasipotimia, msimsikilize,” mnaona, “kwa sababu... msimwogope mtu huyo, kwa sababu sikumtuma kamwe.”

⁶⁹ Hiyo ni busara tu. Mungu akituma chochote, Mungu huunga mkono kile anachotuma; kwa hiyo Mungu akilituma Neno Lake, Mungu huliunga mkono Neno Lake. Sasa, mtu anaweza kuingia na kukwambia lolote. Lakini Mungu anaposema jambo lolote, basi Mungu anaunga mkono yale hasa anayosema atafanya, maana hana budi kufanya hivyo, kusudi awe Mungu. Asingeweza kutoa ahadi halafu asidumu nayo, halafu abaki Mungu, Asingeweza kufanya hivyo, mnaona. Hana budi kudumu na ahadi Yake.

⁷⁰ Sasa, tunaona basi ya kwamba sisi... Mara ya kwanza tunapomwona Yeye akijitokeza jukwaani... Kuna mengi mle ndani ambayo tutayaokota kote katika juma hili, na kuyaingiza ndani kusudi mpate ninii... ufahamu wake zaidi. Lakini hebu tuanze tu na maisha ya Kristo.

⁷¹ Tunajua jinsi alivyozaliwa na bikira, kwenye umri wa—wa miaka thelathini alibatizwa na Yohana Mbatizaji, akaenda nyikani, akajaribiwa na ibilisi siku arobaini mchana na usiku, kisha akatoka na kuanza huduma Yake. Jambo la kwanza tunaloona baada ya Yeye kutoka, vema, Yohana aliona Ishara juu Yake kama nuru. Mfano wa Hua ulishuka kutoka Mbinguni, na Sauti ikitoka kwenye umbo hilo la Hua, Roho wa Mungu, Sauti ikitoka kwa Roho wa Mungu, ambapo huyo Hua alikuwa ni Roho wa Mungu, akisema, “Huyu ni Mwanangu mpendwa ninayependezwa Naye.” Sasa, hilo ni to—toleo la King James. Sasa, katika toleo la asili ni kitu kile kile, lilisema, “ambaye ninapendezwa kukaa ndani Yake,” naye Mungu akakaa ndani ya Kristo, tunajua hilo.

⁷² Yeye alisema, “Si Mimi nizatendaye hizo kazi. Ni Baba Yangu anayekaa ndani Yangu, Yeye huzifanya hizo kazi.” Yohana Mtakatifu 5:19, Yeye alisema, “Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, bali lile amwonalo Baba analitenda, ndilo atendalo Mwana vile vile.”

⁷³ Sasa, “Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake,” sasa, sote tunaamini hilo, ninii... “Mungu alikuwa ndani ya Kristo.” Yeye—Yeye alionyesha kile Mungu alichokuwa, Yeye alikuwa Chapa ya

Mungu iliyodhihirishwa. “Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake.”

Sasa, tunaona ya kwamba wakati alipokuwa hapa, na jinsi watu walivyomjua. . . Sasa, wote aliowajia walikuwa ni waaminio wa Kiyahudi, “Alikuwa kwa walio Wake.”

⁷⁴ Sasa, kuna jamii tatu tu za watu ulimwenguni, acha waseme lolote watakalo, kuna jamii tatu: Watu wa Hamu, Shemu, na Yafethi, maana hizo zilitoka kwa Nuhu, kutoka kwenye safina. Kuna jamii tatu za watu, na kwa hiyo basi, hizo zilikuwa ni Myahudi, Mmataifa, na Msamaria, ambao tunaona ya kwamba Ujumbe wa Kipentekoste uliziendea hizo tatu, ndipo Petro akiwa na zile funguo, na tangu wakati huo na kuendelea ni kwa kila mtu basi. Sasa, tunaona ya kwamba Petro, kwenye siku ya Pentekoste kwa Wayahudi, kisha kuwashukia Wasamaria, wakati Filipino aliposhuka na kuwahubiria huko, na halafu kwenye nyumba ya Kornelio, na basi hiyo hapo. Mnaona? Ulimwengu ukaipata, ukapata Injili.

⁷⁵ Sasa, sasa, hebu na tuangalie, kwa makini sasa, tunapoingia. Sasa, tunamwona Yeye akishuka kutoka nyikani, mara cheche zikaanza kuruka kutoka kwenye huduma Yake, uponyaji ukifanyika, na mambo makuu yakifanyika. Basi ikawa kwamba kulikuwa na mtu jina lake Andrea, alikuwa na ndugu jina lake Simoni. Nilichukua historia ya baba yake, na ya Petro, ambaye tunamjua, usiku wa leo, jina lake wakati huo lilikuwa ni Simoni. Naye Andrea akamshawishi aje kumwona Yesu, na kumwambia Yeye alikuwa ndiye Masihi, alishawishika kabisa ya kwamba huyo alikuwa ndiye Masihi.

⁷⁶ Basi alipomjia Yesu, Yesu alimwangelia. Sasa, kumbukeni, Yeye ni Masihi, na sasa, hivi ndivyo alivyokuwa jana: Na mara alipomwangelia Petro, ama, Simoni, Yeye alisema, “Jina lako ni Simoni nawe ni mwana wa Yona.” Hilo. . . Mara Simoni akalitambua na kumkubali. Sasa, kwa nini mtu huyo, kwa hali hiyo, kwa sababu tu Yesu alisema mambo hayo, “Jina lako ni Simoni nawe ni mwana wa Yona,” naye akamtambua mara moja kwamba ni Masihi, kwa nini afanye hivyo?

⁷⁷ Mnaona, alifundishwa, katika Maandiko, na baba yake, ya kwamba siku moja Masihi atakuja na kutakuwako na vurugu kubwa miongoni mwa watu. Daima kabla ya jambo lililo halisi kutukia, kuna vitu vingi bandia vinavyoinuka kulizunguka, tunajua hilo, daima. Huyo ni ibilisi akijaribu ku—kuliiga, na kumbukeni, mnapoona cha bandia, kumbukeni tu kinazungumza juu ya kuja kwa kilicho halisi, mnaona. Hiyo ni sikuzote. Mnaona?

⁷⁸ Sasa, nami ninaweza tu kumsikia Yona akisema, “Simoni, mvulana wangu,” nywele zake zina mvi, Yona, na kusema, “Daima nilidhani ningeiona siku ambayo Masihi angekuja, lakini ninazeeka sasa, labda sitaiona. Lakini mwanangu, wewe

na Andrea ketini hapa, msisahau, Masihi, kutakuwa na upuuzi mwingi utakaoinuka katika siku zenu, huenda mkamwona. Tumemtazamia, sasa, kwa miaka elfu nne, bali anaweza kuja katika kizazi chenu. Wala msisahau ya kwamba Biblia yetu haiwezi kushindwa, Maandiko yetu hayawezi kushindwa, Yeye atakuwa ni nabii, kwa kuwa Musa, yule tuliyemwamini miaka hii yote, na yule aliyetuongoza kutoka Misri, alitwambia ya kwamba Bwana Mungu wetu atatupa Nabii kama yeye tu, Naye atakuwa Mungu-Nabii, nanyi mtamjua kwa jambo hilo.”

⁷⁹ Basi mara Simoni alipomwona huyu Yesu wa Nazareti akisema, “Jina lako ni Simoni na mwana wa Yona,” yule baba mzee mcha Mungu aliyekuwa amemwagiza, kulikuwako na ishara kamilifu ambayo ilikuwa ni Nabii. Mnaona?

Unajua, walimwambia, “hivi wewe ndiwe Kristo? Hivi wewe ndiwe Nabii *huyu* aliyepaswa kutokea?”

⁸⁰ Sasa, Yeye alijitambulisha Mwenyewe kwa yule mtu ambaye alimpa funguo za Ufalme, ambaye alikuwa ndiye kiongozi wa Kanisa huko Yerusalemu, kwa kumwambia yeye alikuwa ni nani, na jina la baba yake lilikuwa nani. Sasa, hivyo ndivyo alivyojitambulisha Mwenyewe kwa Simoni Petro, naye Petro akamtambua kuwa ndiye Masihi.

⁸¹ Filipo alikuwa amesimama pale, na jambo hilo lilimfurahisha sana, kwa sababu Filipo alikuwa m—m—mtauwa, alikuwa akingojea na kukesha. Mungu. . . Sikilizeni, msisahau jambo hili: Yeye ataonekana tu kwa wale wanaomtazamia, si mwingine. Hiyo ndiyo sababu Yohana aliiona Nuru hiyo, naye ndiye pekee aliyeiona Hiyo, “Yohana alishuhudia akisema, ‘Niliiona.’” Hakuna mtu mwingine aliyeiona. Wakati Paulo alipoiona Nuru iyo hiyo, ikamwangusha chini, Paulo ndiye aliyeiona hiyo Nuru, si hao watu waliokuwa pamoja naye, mnaona. Mnaona? Kumbukeni, ya kwamba Hiyo huwajia wale wanaoitazamia, wanaoiamini. Hiyo ndiyo njia pekee Mungu anayojifunua Mwenyewe, daima amejifunua, na daima atajifunua.

⁸² Angalieni, sasa, Filipo alikuwa amesimama pale. Alipoona jambo hilo likitukia. . . Alijua habari za mtu ambaye walikuwa na shule ya Biblia pamoja, nao walikuwa waorthodoksi, walikuwa kweli wanaamini yale Magombo, nao walikuwa wakitazamia jambo fulani kutukia. Na kuzunguka mlima, kama yeyote wenu aliwahi kuwa Palestina, kutoka mahali ambapo Yesu alikuwa akihubiria, ilikuwa maili kumi na tano kuzunguka kufikia mahali alipompata rafiki yake, Nathanaeli.

⁸³ Nathanaeli alikuwa na shamba la matunda, mizeituni. Na kwa hiyo akaenda mlangoni, na kubisha mlangoni, ndipo mkewe akamwambia kwamba alikuwa huko nje bustanini, kwa hiyo anatoka kwenda bustanini, na huyo hapo Nathanaeli.

⁸⁴ Hebu na tuliingilie, tuone kile alichokuwa akiombea. Ninaweza kuwazia nikimsikia akisema, “Baba, tumemtazamia Masihi, yule Mkombozi, kutuweka huru na mamlaka hii ya Kirumi. Ee, Baba Mungu, hivi nitaishi kuona siku ambayo Masihi huyu atajitambulisha Mwenyewe kwetu? Nimesoma katika Maandiko Yako ambapo Yeye yuaja. Musa alitwambia ya kwamba Bwana Mungu wetu atatuondokeshea Nabii aliye kama yeye, nasi tungemtambua. Na, Baba, ninautamani na kuongojea wakati huo. Nimeyasoma Maandiko; nimeishi ndani Yao mchana na usiku.”

⁸⁵ Ndipo yapata wakati aliposema, “Amina,” na kusimama, Filipo akasema, “Njoo, umwone Yule tuliyemwona. Tulimwona Yeye, Yesu wa Nazareti, mwana wa Yusufu.”

⁸⁶ Vema, ninaweza kumwazia Nathanaeli, sasa, nitatoa mchezo mdogo tu wa kuigiza, ninaweza kuwazia Nathanaeli akisema, “Sasa, Filipo, nimekujua kuwa mtu mwenye akili timamu sana. Nami... Hakika, hujapata wazimu wa jambo fulani,” mwajua, kama vile tungesema leo. “Sasa, Filipo, tumesoma Maandiko kupita kiasi pamoja. Sasa, wewe unakuja kuniambia ya kwamba Masihi yupo hapa, sasa, unajua vizuri na dhahiri kama Masihi huyo akija, Yeye angetujia sisi Mafarisayo peke yetu, kundi letu, na hilo pekee. Ama Yeye angeninii... Wangeutandaza ushoroba, Naye angeshuka hekaluni kwenye lile hekalu kuu ambalo Musa alijenga, Naye angejitambulisha Mwenyewe kwa Kayafa Kuhani Mkuu, ‘Mimi ndimi yule Masihi mneyemtafuta.’”

⁸⁷ Mnaona? Hivyo ndivyo huenda walikuwa wameyapanga yote, lakini Mungu ana njia Yake Mwenyewe ya kufanya mambo, mnaona. Mnaona? Yeye alikuja sawasawa kabisa na Maandiko, bali wao waliyafasiri Maandiko vibaya. Sijui kama Yeye akija... kama angekuja usiku wa leo, kama wengi wetu hatujachanganyikiwa kabisa. Lakini jambo muhimu ni: Iweni tayari wakati atakapokuja, ja—jambo ndilo hilo, haidhuru Mungu anamtuma kwa njia gani. Mwacheni tu aje jinsi Yeye—jinsi Yeye—Yeye alivyompangia kuja. Baadhi yetu wanaye akija juu ya wingu jeupe, wengine juu ya farasi mweupe, sijali jinsi anavyokuja, maadamu niko tayari atakapokuja, na—na—nataka kumwona. Nami ninasoma kwa bidii kujua yale hasa Maandiko yasemayo, kwa hiyo nitamjua atakapotokea, mnaona. Angalia yale Maandiko yasemayo kumhusu Yeye.

⁸⁸ Sasa, yeye alisema, “Njoo uone Yule tuliyemwona.” Vema, bila shaka mazungumzo yakaendelea, na hebu tuyaingilie, wanapozunguka ukingoni. Nililitoa katika... Yeye labda siku moja aliuzunguka huo mlima, akarudi kesho yake. Na kesho yake akiwepo alisema... Naweza kumsikia Filipo akimwambia Nathanaeli, “Nathanaeli, unakumbuka wakati ule ulipowanunua wale samaki kutoka kwa maskini jamaa yule mzee, aliyelitwa Simoni?”

“Loo, naam, mwana wa Yona, hakika.”

“Unajua, hata hakuwa na elimu ya kutosha kukutilia ririsiti sahihi, risiti kwamba amewanunua hao samaki.”

⁸⁹ “Naam.” Mnaona, Biblia ilisema Petro alikuwa mtu asiye na elimu wala maarifa. Ni wangapi wanaojua hilo? Naam, bwana. Hakuwa na elimu, hakuwa msomi fulani wa seminari, na yeye—yeye alikuwa ni mtu asiye na elimu wala maarifa.

⁹⁰ Kisha kasema, “Asingeweza kutia sahihi risiti hiyo. Mbona,” kasema, “alipokuja kwa nanii wake . . . mwaliko wa ndugu yake Andrea, naye akaja mbele ya huyu, Ambaye tunamjua kuwa ndiye Masihi. . . Nami nitawaambia ni kwa nini ninajua hilo. Sasa, mnajua, Nathanaeli, ya kwamba mimi na wewe tunajua Maandiko yanasema ya kwamba Yeye atakuwa ni Nabii kama Musa. Basi mara alipoenda mbele za Yesu, Yesu alisema, ‘Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona.’ Sasa, angejua je hilo kama hakuwa nabii?”

⁹¹ Nami namsikia Filipo akisema, “Unajua, Nathanaeli, haitanishangaza hata kidogo, ila, utakapokuja mbele Zake, Yeye hatasema, ‘Habari za jioni, Nathanaeli.’”

⁹² “Ah,” anasema, “ah,” Nathanaeli anasema, “hebu niende nikajionee mwenyewe.” Hilo ni wazo zuri, mwajua. Na, kwanza ilikuwa vigumu kwake kuamini, naye akaalikwa aje ajionee mwenyewe. Kasema, “Laweza neno lolote jema kutoka Nazareti, kundi hilo la watakatifu wanaojiviringi- . . .,” ama, mwajua, “watu kule chini?” Samahani. “Je, laweza neno lolote jema kutoka huko?”

⁹³ Akasema, “Njoo, ujionee mwenyewe.” Usikae nyumbani na kulikoso, njoo, ujionee. Njoo, uone. Wala usichukue tu neno la huyo mtu, lichunguze uone kama ni la Kimaandiko au la, unaona. “Njoo, ujionee mwenyewe.” Nao wakienda zao walizungumza.

⁹⁴ Hatimaye, wakafika mahali ambapo Yesu alikuwa na ibada ya uponyaji. Wao . . . Huenda Nathanaeli alikuwa kwenye mstari wa maombi, sijui, ama huenda alikuwa amesimama kwenye kusanyiko, lakini wakati alipomwona Yesu kwa mara ya kwanza, naye Yesu akamtazama, alisema, “Tazama Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake!” Hilo lilimnyong’onyesha kabisa, kama isemwavyo. Yeye . . . Mbona, ali- . . . asingeweza kuelewa!

Akasema, “Rabi,” ambalo linamaanisha, “mwalimu,” “ulipataje kunijua Wewe? Hii ndiyo mara ya kwanza tumewahi kukutana. Ungenijua je Wewe?”

Naye akasema, “Mbona, kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona.” Maili kumi na tano kuizunguka milima, ni macho ya jinsi gani! “Nilikuona.”

⁹⁵ Upesi mtu huyo akatambua ya kwamba huyo . . . Hawakuwa na nabii kwa muda wa miaka mia nne, mwajua, naye akatambua

mara moja huyo alikuwa Ndiye. Kwa hiyo akamkimbilia na kusema, “Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu; Wewe ndiwe Mfalme wa Israeli.” Hiyo ni kweli?

Akasema, “Kwa sababu nilikwambia hivyo, uliamini?”

⁹⁶ Kwa nini? Sasa, huyo alikuwa ni Yesu jana. Kama ni yeye yule leo, angefanya jambo lile lile, mnaona, kama Yeye ni yule yule jana. Hivyo ndivyo alivyojitambulisha Mwenyewe kwa watu Wake, hivyo ndivyo walivyomtambua, si kwa mafundisho Yake, kwa kazi Zake. Mnaona?

⁹⁷ Yesu alisema, “Yachunguzeni Maandiko; Hayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi, ndani Yake mnadhani mna Uzima wa Milele, Nayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi. Na kama sizitendi kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi. Lakini kama nikizitenda kazi za Baba Yangu, nanyi hamwezi kuniamini Mimi, vema, basi aminini kazi nizifanyazo, hizo ndizo zinazonishuhudia Mimi.” Matendo, thibitisho la Neno, hilo ndilo linaloshuhudia. Vema, si lingekuwa ni jambo lile lile leo? Kazi zinashuhudia. Hili *hapa* Neno linalosema hivyo, na hizi *hapa* kazi zinazolishuhudia hilo Neno. Sasa, Yeye hawezi kubadilika, hana budi kuwa yeye yule.

⁹⁸ Sasa, loo, hao hapo wamesimama pale, hakika, wamesimama pale nyuma, yule Kuhani Mkuu mashuhuri, na makuhani wa masinagogi, na hao wote wamesimama pale wakiangalia, na, bila shaka, iliwabidi kutoa jibu kwa kusanyiko lao, ni . . . kazi ilikuwa imefanywa.

Unajua walichosema? Walisema, “Yeye ni Beelzebuli, mpiga ramli, ibilisi.”

⁹⁹ Ndipo Yesu akageuka na kuwaambia hivi: “Amin, amin, nawaambia,” mnaona, “mkisema hayo dhidi ya Mwana wa Adamu, nitawasamehe. Lakini,” vinginevyo, “siku moja Roho Mtakatifu atakuja kufanya kazi ile ile, na kunena neno moja dhidi Yake, hakutasamehewa kamwe, katika ulimwengu huu, wala ulimwengu ujao.”

¹⁰⁰ Sasa, mnaona? Mnaona? Angalieni unabii huo ukiingia katika siku zetu, mnaona, “kusema neno dhidi Yake, hakutasamehewa kamwe, katika ulimwengu huu, wala katika ulimwengu ujao.”

¹⁰¹ Naye huyu hapa Filipo, Petro, na hao wengine wamesimama pale, hao Wayahudi wakisema, “Yeye ni Mwana wa Mungu; Mfalme wa Israeli,” kwa sababu Yeye alifanya mambo hayo mbele yao. Na lile, linavyodhaniwa kuwa, la kiothodoksi lilisema, “Yeye ni Beelzebuli, ibilisi, mpiga ramli.” Mnaona?

¹⁰² Naye Yesu alishuhudia ya kwamba hilo lingekuwa katika siku nyingine, kwa Roho Mtakatifu, maana Roho Mtakatifu hakuwa ametolewa wakati huo, Yeye alikuwa bado hajatolewa dhahihu. Kwa hiyo Roho Mtakatifu angekuja, na kunena dhidi Yake basi

kwa sababu... Ni kitu gani? Kumwita Roho wa Mungu, ambaye anafanya kazi za Mungu, roho mchafu, ibilisi. Mnaona? Sasa, imetabiriwa na Yesu Kristo ya kwamba ingetukia hivyo, na haina budi kuwa hivyo.

¹⁰³ Sasa, hebu na tumwone Yeye. Sasa, kumbukeni, kuna jamii tatu za watu, hizo zilikuwa watu wa Hamu, Shemu, na Yafethi. Rangi zetu zilibadilishwa na ma... nchi tulizoishi, na—na kadhalika, na hilo halina chochote, fanya... Mungu aliwafanya kwa damu moja, mataifa yote. Awe Mchina, Mjapani, au Mwafrika, au Mwanglo-Sakson, ama chochote alichio, wote ni damu moja, wote walitoka kwa Adamu, mnaona. Nao wamelelewa katika sehemu mbalimbali za nchi na nchi zenye joto.

¹⁰⁴ Sasa, chukua tu chochote, kitafanya jambo lile lile. Unaweza kumchukua mbwa mwitu huko chini Mexico, na umwache aishi kwenye ardhi hiyo ya mchanga mwekundu, yeye ni wa rangi nyekundu, mlete huku juu, kwenye mchanga mweupe, ana rangi nyeupe, kidogo ni hudhurungi, mpeleke huko juu, huko juu kabisa katika nchi ya kaskazini, huko juu kabisa katika British Columbia, yeye ni mweupe kama theluji, mbwa mwitu yule yule, hasa.

¹⁰⁵ Kulungu yule yule atabadilika rangi kutoka nyekundu, kahawia, na nyeusi. Naam, bwana. Inategemea nchi anamoishi, chakula anachokula, na kadhalika namna hiyo. Sasa, hivyo ndivyo rangi zetu na kadhalika zilivyobadilika, bali sote tunatoka katika jamii moja. Hiyo ni jamii ya binadamu, hiyo ni kweli, wote wametoka kwenye mti huo mmoja.

¹⁰⁶ Sasa, kulikuwako—kulikuwako na Wayahudi. Alikuwa kwa hao Wayahudi kwa sababu walikuwa wakimtazamia Masihi. Sasa, tuna wengine kadhaa hapo tutakaowapitia katika hizi sehemu za juma, nasi tutaninii, muda uliosalia wa juma hili, tutawapitia, na kadhalika, lakini chukueni tu... wachukueni tu hao wawili hapo, Petro na mtu huyu, Nathanaeli. Na hivyo ndivyo walivyojua ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi.

¹⁰⁷ Sasa, siku moja alihitaji kupitia Samaria. Sasa, huyo ni Msamaria, ambaye ni jamii nyingine ya watu, na ilimbidi kupanda juu... Alikuwa akienda zake Yeriko, kushuka chini moja kwa moja, bali akazunguka huko Sikari, huko pamoja na... Samaria, akasimama kwenye mji fulani, Sikari. Ndipo akawatuma wanafunzi Wake kununua chakula.

¹⁰⁸ Nao walipokuwa huko, mwanamke, vema, tungemwita mwanamke mwenye sifa mbaya hapa katika nchi hii, alikuwa ameolewa mara kadhaa na kadhalika, naye alikuwa... akaja kisimani, yapata, nadhani, yapata wakati wa adhuhuri, wakati alipowatuma wakanunue chakula cha mchana, naye akaja kisimani.

¹⁰⁹ Na kuna ninii... Hicho kisima kingalipo. Ni mandhari ya kitu kama *hiki* na mizabibu juu yake, na kuna mji, kisima cha umma pale, ambapo watu huja kuteka maji. Basi alipokuja kwenye kisima hiki, yapata saa tano, na labda ninii zake zote, mwajua, hao akina mama, jinsi walivyopinda nywele zao na, mwajua, na kadhalika... Naye angeninii... Huenda ikawa alikuwa nje usiku kucha na ndio kwanza aamke, kwa hiyo sijui ilikuwaje, lakini alitoka.

¹¹⁰ Nanyi laiti mngaliwaona hao wanawake huko, jinsi wanavyoweza kuyabeba hayo maji! Nimewaona wakiweka mtungi wa galoni tano juu ya kichwa chao, na mmoja kwenye kila nyonga, na kushuka kwenda mtaani, wakiongea tu kama vile kina mama wanavyoweza kuongea, mwajua, wakitikisa vichwa vyao mmoja kwa mwingine, na kamwe wasimwage tone moja. Nena kuhusu kutembea kikamilifu!

¹¹¹ Na kwa hiyo mwanamke huyu, asingeweza kutoka pamoja na wanawake wengine, mnaona, kwa sababu alikuwa ametiwa alama. Katika nchi yetu hawatiwi alama, lakini huko wanatiwa. Wao... Hawezi kushirikiana na wanawake wengine mradi anaishi hivyo, kwa hiyo asingeweza kuja wakati uo huo wale wanawali walipokuja.

¹¹² Kwa hiyo akatoka yapata saa tano. Na kuna ki-kisima pale, na winchi, naye alikuwa na ninii... Kulabu zinaingia kwenye... gudulia hili kubwa, lina viopoo juu yake, tunaliita gudulia, waliliita ndoo wakati huo, nadhani, waliliwekelea juu, na wakaanza tu kulishusha, ndipo akamsikia Mtu fulani akisema, "Mwanamke, nipe maji ninywe," ndipo akaangalia kugemea ukutani, na hapo ameketi Myahudi mwenye umri wa makamu.

¹¹³ Sasa, tunajua ya kwamba Yeye alikuwa kweli, kulingana na Maandiko, alikuwa na yapata tu, hajapata thelathini na mitatu, lakini hapana shaka alionekana mzee kidogo. Unajua katika Yohana Mtakatifu mlango wa 6, walimwambia, kasema, "Wewe ni mtu asiyezidi umri wa miaka hamsini, nawe wasema umemwona Ibrahimu? Sasa tunajua una pepo."

Akasema, "Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO." Unaona? Unaona, Yeye alionekana wa hamsini kulingana nao, bali Yeye... Huenda kazi Yake ilimlelea sana.

Naye alikuwa ameketi karibu na kisima, kasema, "Nipe maji ninywe."

¹¹⁴ Vema, huyo mwanamke, pasipo kuwazia chochote, mwajua, labda, mwanamke, mfano wa huyo, akasema, "Bwana, si kawaida Kwako, Myahudi, kuniomba mimi, mwanamke Msamaria, chochote, maana hatuna uhusiano sisi kwa sisi." Ubaguzi, mnaona?

¹¹⁵ Naye akawajulisha upesi sana ya kwamba kwa Mungu hakukuwa na ubaguzi, kwa hiyo, na kwa hiyo, Yeye alinena

naye na kusema, “Kama ungalijua ni Nani unayesema Naye, ungeniomba Mimi maji unywe, ningekuletea Maji usije hapa kuchota.”

Akasema, “Kisima ni kirefu, Nawe una . . .”

¹¹⁶ Alikuwa akifanya nini? Sasa, Yeye alikuwa akiwasiliana na roho yake. Mnaona? Alikuwa shika- . . . Sasa, Yeye alisema alikuwa na haja ya kwenda kule juu, Baba alimtuma, kwa hiyo alikuwa na haja ya kupitia kule. Sasa, hili hapa somo, bila kujua atakalofanya, maana Yohana Mtakatifu 5:19 ilisema Yeye hakufanya lolote mpaka Baba alipomwonyesha. Lakini sasa hana budi kutafuta, kile mwanamke huyu . . . ? Labda Baba alikuwa amemwonyesha aende kule, na sasa Huyu hapa, Yeye hajui la kufanya, lakini huyu hapa mwanamke akijitokeza. Sasa, Yeye hana budi kuwasiliana na roho yake. Loo, natumaini mnalion!

¹¹⁷ Na kwa hiyo, basi Yeye anazungumza naye, anaendelea na mazungumzo, ndipo hatimaye Yeye . . . Walianza kuzungumza juu ya mahali pa kuabudia, na makabila yao mbalimbali ama madhehebu, na kadhalika, Naye akasema, “Wote . . . Baba anawatafuta watu kama hao wamwabudu katika Roho na Kweli.” Kwa hiyo hatimaye, akajua shida yake ilikuwa ni nini, Naye akamwambia, “Nenda, kamwite mumeo, mje naye hapa.”

Akasema, “Sina mume.”

Kasema, “Umesema vema, kwa kuwa umekuwa na watano; na yule unayeishi naye si wako.” Jamani!

¹¹⁸ Angalia, angalieni tofauti kati ya mwanamke huyu mwenye sifa mbaya na hao makuhani. Hao makuhani, wakati hilo lilipofanywa, walisema, “Yeye ni Beelzebuli, mpiga ramli.”

¹¹⁹ Lakini maskini mwanamke huyu mwenye sifa mbaya, alisema, “Bwana, naona kwamba Wewe ni Nabii.” Loo! “Sisi,” sisi Wasamaria, “tunajua Masihi yuaja, aitwaye Kristo, na atakapokuja, hii itakuwa ndiyo ishara Yake. Hivyo ndivyo atakavyofanya.”

¹²⁰ Kumbukeni, Yeye hakufanya hivyo hata wakati mmoja mbele ya Mataifa, hawakuwa wakimtazamia Masihi yeyote, hii ndiyo siku yao, mnaona. Wao, Wayahudi na Wasamaria, walikuwa wakimtazamia Mmataifa, kwa sababu Myahudi alikuwa nusu Myahudi na—na Mmataifa, ambalo lilifanya Msamaria.

¹²¹ Kwa hiyo akasema . . . Sasa, angalia. Akamwambia huyu . . . “Naona ya kuwa Wewe ni Nabii. Tunajua ajapo Masihi, aitwaye Kristo, hiyo itakuwa ndiyo ishara Yake. Yeye atatuonyesha mambo haya atakapokuja.”

Naye Yesu akasema, “Mimi ninayesema nawe Ndiye.”

¹²² Huyu akaenda zake mjini, basi usikilizeni ujumbe wake, “Njoni, mwone Mtu ambaye ameniambia mambo niliyofanya.

Haimkini huyu kuwa ndiye Masihi?” Vema, kama ni yeye yule jana, leo, na hata milele! Si ni kweli? Nayo Ma—Maandiko yanasema ya kwamba watu . . . Yeye hakufanya hivyo tena. Ma—Maandiko yanasema ya kwamba watu walimwamini kwa sababu ya neno la mwanamke huyo, kwa sababu walijua hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi. Na Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Hiyo ni kweli. Sasa, Yeye ni . . . Aliona hiyo kuwa ndiyo ishara ya Masihi, Wayahudi waliiona kuwa ndiyo ishara ya Masihi.

¹²³ Sasa, kusukumia tu ndani, yapata dakika tano tu zaidi, juu ya jambo moja zaidi. Yesu alisema kabla ya kuja kwa Mwana wa Adamu, ingekuja siku kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma.

¹²⁴ Sasa, kumbukeni, daima kumbukeni hili: Mungu yuko katika tatu, mwajua, tarakimu Za—Zake. Mungu anakamilika katika tatu kama vile, Baba, Mwana, Roho Mtakatifu, na kadhalika. Sasa, angalieni: tatu. Sasa, daima kuna matabaka matatu ya watu, kama vile Hamu, Shemu, na Yafethi. Na kuna matabaka matatu ya watu yanayoketi pamoja kwa kawaida, hayo ni waaminio, wanaojifanya waaminio, na wasioamini. Mnao hao kila mahali. Nanyi mnao. Sasa, na daima kumekuwa na hiyo . . . Sasa, angalieni hapa, Yesu akiufananisha mfano wa Sodoma, kama ilivyokuwa, itakuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu.

¹²⁵ Sasa angalieni, Lutu alikuwa ni jamaa, mpwa, wa Ibrahimu. Labda juma hili tutamwingilia Ibrahimu na baadhi ya kazi zake. Sasa, nasi tunaona ya kwamba Lutu aliondoka akaingia ulimwenguni, katika Sodoma, kuishi, loo, pamoja na, vema, mambo ya ulimwengu. Akawa mtu mkuu wa mji, labda meya, ama ninii . . . aliketi . . . alikuwa ndiye hakimu, aliketi langoni na kuwahukumu watu, mkewe alikuwa ni mfuasi wa kila shirika lililokuwako mjini, hata hivyo alikuwa na mguso wa Mungu.

¹²⁶ Huo ni mfano, wakati wa mwisho, wa kanisa lililoko ulimwenguni, lingali linaishi katika mambo ya ulimwengu, kanisa la kawaida, halafu kulikuwa na Msodoma, ambaye ninii watu hapa mnajua kile walichokuwa. Sasa, kulikuwako . . . Ibrahimu alikuwa ni mfano wa Kanisa lililoitwa litoke, hakuwa Sodoma, ameketi nyuma kabisa *hapa* juu kwenye maeneo kame ya mlima, juu ya utajiri na shughuli za ulimwengu. Hayo hapo matabaka yako matatu.

¹²⁷ Ibrahimu, aliyeitwa atoke, nalo neno *kanisa* linamaanisha “aliyeitwa atoke,” Ibrahimu, Kanisa teule. Tunajua kuna Kanisa teule, tunajua hilo. Mungu alichagua Kanisa tangu zamani, litaonekana mbele Zake bila waa wala kunyanzi, Yeye alisema hivyo; natumaini mimi ni mshiriki Wake. Nami ninajua jinsi unavyopata kuwa mfuasi Wake: kwa kufa kwa nafsi yako, na kuzaliwa Kwalo. Hivyo tu.

128 Sasa, lakini Kanisa teule, Biblia ilisema katika siku za mwisho mpinga-Kristo angewadanganya walio hasa Wateule, kama yamkini, bali haiwezekani, mnaona, “kama yamkini.” Sasa, angalieni, hao hapo Wasodoma; huyo hapo Lutu, mwenye uvuguvugu; kisha huyu hapa Ibrahimu ameketi hapa nje kwenye haya maeneo kame.

129 Sasa, siku moja kukatokea Wageni watatu, na hao Wageni watatu walionekana kama wanaume, Walikuwa na mavumbi kwenye nguo Zao, Wakaketi pamoja na Ibrahimu, naye Ibrahimu akaenda akachinja ndama, na kuchukua ugali wa mahindi, na maziwa, na vipande vya nyama ya ndama, akatoka nje na kuwalisha Viumbe hawa wa Kimalaika, Nao wakala. Angalieni, nao Hawa hapa, ndipo wawili kati Yao wakashuka kwenda Sodoma kuhubiria Sodoma, Yule aliyebaki nyuma akazungumza na Ibrahimu.

130 Sasa, hebu tuchukue tu leo. Sasa, si ni ajabu kwamba kanisa la kawaida, huko nje katika u—ulimwengu wa kimadhehebu, wamekuwa na mlipuko mkubwa, wahudumu wawili mashuhuri? Si ni ajabu kwamba A-b-e-r-h-a-m na G-r-a-h-a-m hayajawahi kusikika hapo awali ulimwenguni kote? Halafu tuko na Ndugu Oral Roberts, mtu mwingine mashuhuri. Basi kumbukeni kama vile G-r-... , ama, Malaika hawa walishuka wakaingia Sodoma, hawakufanya miujiza yoyote, ila usiku mmoja walipofushwa, nako kuhubiriwa kwa Neno humpofusha asiyeamini, anapofushwa na Neno.

131 Sasa, hebu na tumwangelie Huyu aliyelhubiria Kanisa teule. Angalia, yapata siku moja ama mbili hapo kabla, Abram alibadilishwa jina lake kutoka Abram likawa Ibrahimu, naye Sarai, S-a-r-r-a, likawa S-a-r-a, Sara, “binti mfalme.” Ndipo wakati Huyu aliyekaa na Ibrahimu, Yeye alikuwa ameelekeza mgongo Wake kwenye hema, Naye akasema, “Ibrahimu, yu wapi Sara, mkeo?” S-a-r-r-a, ni Sara, “binti mfalme,” alijuaje ya kwamba yeye... ya kwamba Mungu alikuwa amebadilisha jina lake, siku moja au mbili hapo kabla, kutoka Abram likawa Ibrahimu, nalo jina la mke kutoka Sarai likawa Sara? Mnaona? Angalieni sasa. Naye alijuaje hata alikuwa ameo? Naye alijuaje alikuwa na mke? Wanawake wakati huo hawakukimbia na kuchukua mahali pa wanaume kama wafanyavyo siku hizi, walikaa ndani, jikoni ambapo palikuwa mahali pao. Lakini basi... Lakini imebadilika tangu wakati huo, sana.

Na kwa hiyo, basi tunaona ya kwamba alikuwa huko nyuma hemani, kasema, “Yu wapi Sara, mkeo?”

Basi kumbukeni, Ibrahimu alisema hasa, sasa, “Yuko hemani nyuma Yako.”

132 Naye akasema, “Ibrahimu, mimi nitakujia,” hiyo *mimi*, hicho kiwakilishi nafsi, hiyo inaonyesha Yeye alikuwa ni Nani, papo hapo, “Nitakurudia kulingana na wakati wa uhai.”

¹³³ Sasa, sisi ni kusanyiko lililochanganyikana, nyinyi humsikiliza daktari wenu, mimi ni ndugu yenu. Sasa, walikuwa wazee, Ibrahimu alikuwa na umri wa miaka mia moja, naye Sara alikuwa na tisini. Sasa, kama mume na mke, ilikuwa imekoma, labda miaka kumi, kumi na mitano, ishirini kabla ya hapo, hawakuwa na uhusiano tena kama mume na mke.

¹³⁴ Naye Sara akaguna, kile tunachokiita huko Kentucky, nyote mnakiita hapa “tabasamu,” ama chochote kile, “akachekeka kifichifichi,” nafikiri huo ndio msemu. Akasema, “Mimi,” sasa, si kwa sauti, “mimi,” akasema, “mwanamke mkongwe, na bwana wangu,” ambaye alikuwa ni Ibrahimu, mumewe, “mzee pia, ati tungepata raha tena?” kama vijana, mwajua. “Mimi, mwanamke mkongwe namna *hii*, naye ni mzee namna *hiyo*?” Akachekeka.

¹³⁵ Naye Malaika, huku mgongo Wake umeelekezwa kwenye hema, akasema, “Kwa nini Sara akachekeka? Akisema juu ya haya...” Ni telepathia ya aina gani hiyo? Angalieni, Mungu angaliuchukua uhai wa Sara papo hapo, bali asingeweza, yeye alikuwa ni sehemu ya Ibrahimu. Na hilo ni jambo lile lile kwa Kanisa siku hizi, mnaona, kutokuamini kwetu kwote na kadhalika, Yeye angetuondoa duniani, bali hawezi, sisi ni sehemu ya Kristo, mnaona, kwa hiyo Yeye hutusamehe dhambi zetu, mnaona. Angalimchukua. Tutaingilia mambo hayo kindani zaidi baadaye, maana wakati wetu unakwisha, lakini angalieni.

¹³⁶ Sasa, Yesu alisema... Sasa, ulisema, “Mtu huyo alikuwa ni nani? Alikuwa ni nani?” Ibrahimu anapaswa kujua, Ibrahimu alimwita “Elohimu.” Hiyo ni kweli? “Anayeishi peke Yake,” Mungu Mwenyewe aliyefanyika mwili, na kuonyesha ya kwamba Mungu, katika siku za mwisho, Yeye alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu,” kwamba Mungu, Mwenyewe, katika Umbo la Roho Mtakatifu, angekuwa sana Kanisani Mwake, limejazwa sana, hata angekuwa akitembea na kufanya kazi Kanisani. Mungu katika mwili wa kibinadamu, unaona, akifanya jambo lile lile.

¹³⁷ Sasa, kama Wayahudi walikuwa na ishara hiyo ya—ya Masihi mwishoni mwa wakati wao, na Wasamaria mwishoni mwa wakati wao, maana walikuwa wakiangalia... Tumekuwa na miaka elfu mbili ya kuhubiri, theolojia, haijawahi kuwako Kanisani kamwe hapo kabla, na sasa, hapa katika siku za mwisho, kule kumalizia, kwa ahadi ya Kristo na mamia ya ahadi zaidi kwamba mambo haya yangetukia, basi kama tungetaka kumwona na kutaka kujua Yeye ni Nani, hana budi kuwa yeye yule jana, leo, na hata milele. Hiyo ni kweli. Inapaswa kuwa vivyo hivyo, Yesu aliahidi vivyo hivyo, basi, “Mabwana, Sisi Tunataka Kumwona Yesu.”

¹³⁸ Ungemjua? Kama ningeshuka kwenda Santa Maria, usiku wa leo, na kumwona mtu aliyekuwa amevalia kama Yeye,

amevaa makubadhi, na labda amevaa joho, na amejaa makovu usoni mwake namna *hii*, na alama za misumari, mkononi mwake, huyo angeweza kuwa ndiye mnafiki mkubwa kuliko wote nchini. Mtu yeyote angeweza kuiga hilo. Bila shaka.

¹³⁹ Lakini unaujuaje mti? Yesu alisema ungewajuaje? Kwa tunda lao. Sasa, ninyi watu ni—ni wakulima wa machungwa hapa. Sasa, vipi kama mlichukua... kama mngeweza kutoa uhai wote katika mchungwa na kuuweka kwenye... na kutoa uhai wote kutoka kwenye mba—mbalungi, na kutia uhai wa mchungwa kwenye mbalungi, ungezaa nini? Machungwa. Hakika. Uhai ulio ndani yake ndio unaozaa kile ulicho. Hiyo ni kweli? Sasa, simaanishi kupandikiza sasa, ninamaanisha kuutoa huo uhai. Hiyo ndiyo shida siku hizi, mna kupandikiza kwingi kupita kiasi, wala hakuna kufa kwa kutosha na kutoa uhai, ndipo Uhai mpya uzaliwe humo ndani, hivyo ndivyo ilivyo.

¹⁴⁰ Lakini wakati maisha mapya... Kama ungetoa u—uhai kutoka kwenye boga na kuuweka kwenye mzabibu, na kutoa uhai wa huo mzabibu, mzabibu ungezaa maboga, maana huo ndio uhai ulio ndani yake. Hakika ungezaa, ni uhai ulioko mle ndani. Uhai ulioko Kanisani ndio unaoleta kile lilicho. Mnaona?

¹⁴¹ Sasa, Uhai Wake, katika siku hizi za mwisho, uko Kanisani Mwake, naye “Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele.” Tunaamini hilo, sivyo? Sasa, kama Yeye amekuja katika mfano huu apate kuonekana hapa kwenye Kanisa la Mataifa linalomtazamia Yeye kuja... Sasa, kama akiliacha Kanisa liendeleo moja kwa moja liingie kwenye theolojia peke yake, basi aliwafanyia Wayahudi na Wasamaria jambo fulani lililomfanya tofauti siku hizi. Yeye—Yeye—Yeye ali—... Yeye hakututembelea namna hiyo, hawezi kufanya hivyo. Mnaona? Uamuzi Wake wa kwanza, jinsi ya kujitangaza Mwenyewe, hivyo ndivyo alivyofanya mara ya pili, na hivyo ndivyo atakavyofanya mara ya tatu, kwa kuwa Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Hiyo ni kweli. Unaamini hilo? Amina.

Sasa, ningeweza kuzungumza usiku kucha. Tayari wakati wangu wa kufunga umewadia, lakini tutauweka katika siku zingine usiku.

¹⁴² Yachunguzeni Maandiko hayo mtakapoenda nyumbani, mwone kama Mungu aliliahidi. Angalieni kama hiyo ndiyo njia... Nionyesheni njia yoyote ambayo Yeye alijitambulisha Mwenyewe kwayo, njia nyingine yoyote isipokuwa njia hiyo, kwa sababu Biblia ilitangaza ya kwamba Yeye angekuwa nabii.

¹⁴³ Sasa, ninaamini ya kwamba, siku hizi, Roho Mtakatifu amekuja juu ya Kanisa. Ninaamini alikuja kurejesha yote yaliyoliwa na tunutu, na parare, na kadhalika kote katika nyakati za giza. Na sasa, amekuwa akijenga mpaka liko moja kwa moja hapa kwenye wakati wa kichwa sasa, kwa kuwa Nuru za jioni ni ahadi ya nabii, kwamba itakuwa nuru wakati wa jioni.

144 Ustaarabu umesafiri pamoja na jua. Jua lilichomoza mashariki, kisha jua lilo hilo, j-u-a, linalochomoza mashariki ndilo j-u-a lile lile linalotua magharibi. Tumekuwa na siku yenye utusitusi, kama Biblia ilivyosema, “haiitwi mchana wala usiku,” ya kutosha kujiunga na kanisa, na kutenda mema, na kadhalika, “lakini itakuwa nuru wakati wa jioni.”

145 Basi M-w-a-n-a yule yule, Mwana wa Mungu, aliyeinuka huko mashariki juu ya watu wa mashariki, na kuonyesha baraka Zake na nguvu, imekuwa siku yenye utusitusi, lakini sasa kwenye Pwani ya Magharibi, kama tukienda mbali zaidi, tutarudi Uchina tena mashariki, na kurudi kwenye nchi ya mashariki.

146 Sasa, tuko kwenye Pwani ya Magharibi, Naye M-w-a-n-a anaonekana kabla ya kuja Kwake. Kumbukeni, *kuonekana* na *kuja* ni maneno mawili tofauti. Mnaona? Anaonekana sasa Kanisani, akijionyesha Mwenyewe kuwa hai baada ya miaka elfu mbili. “Mabwana, Sisi Tunataka Kumwona Yesu.”

147 Sasa, kama ninyi waaminio...Ni waaminio wangapi waliopo hapa? Kama...Nisingeweza kufanya hivyo, siwezi kumleta, inatuhitaji sisi sote pamoja kufanya hivyo. Mimi ni sehemu Yake tu, nawe ni sehemu Yake. Lakini kama wewe ni mgonjwa na mhitaji...Mimi ni ndugu yako. Nao... Mungu aliweka Kanisani...Sasa, kuna karama tisa za kiroho zinazolingia katika kila mwili wa mahali hapo, ambazo ni lugha, tafsiri za lugha, na unabii, na kadhalika. Lakini kuna ofisi tano zilizochaguliwa tangu zamani za Kanisa: mitume, manabii, waalimu, wachungaji na wainjilisti; hizo ndizo Mungu alizoweka Kanisani. Roho Mtakatifu...Hiyo ni ofisi.

148 Huenda Roho Mtakatifu akamshukia mmoja usiku wa leo, na kunena kwa lugha, na mwingine atoe unabii, na—na kadhalika, halafu usiku unaofuata huenda akawa juu ya mtu mwingine, na mtu mwingine, namna hiyo, hizo ni karama za mahali hapo kwenye mwili kutuweka sawa. Lakini katika Kanisa pekee, ofisi tano: mitume (maana yake ni “wamishenari”), mitume, manabii, waalimu, wachungaji, na wainjilisti, Mungu huwaweka hao Kanisani.

149 Sasa, hebu na tuamini kwa moyo wetu wote kwamba kupitia karama hizi za huduma kwamba Mungu mkuu wa Mbinguni atamtuma Kristo miongoni mwetu, usiku wa leo, kwamba tutamwona Yesu. Na tuombe sasa tunapoinamisha vichwa vyetu.

150 Baba Mwenye Neema sana, ambaye tumekuwa Kwake kuishi katika hema Lake, kuishi hapa katika uchumi mkuu wa Mungu duniani, na kuongozwa hapa kama ilivyo Mbinguni, jalia Ufalme wa Mungu uje na mapenzi ya Mungu yatendeke miongoni mwetu, usiku wa leo. Tujalie, Baba.

151 Na kama...Maneno machache tu kutoka Kwako, ama Neno moja kutoka Kwako baada ya mimi kunukuu ahadi Zako nyingi

sana usiku wa leo, ila watu tu wanangojea kukuona Wewe ukisema hivyo, Neno Lako lita—litalithibitisha, Baba.

¹⁵² Sasa, maneno yangu, ninaweza tu kusema yale uliyosema Wewe, lakini sasa, kama Wewe utasema tu ni kweli, Bwana, kwa kulithibitisha Neno, basi tutaondoka hapa, usiku wa leo, kama tu wale waliotoka Emau, kama tulivyoomba katika maombi yetu ya awali, tukisema, “Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu?”

¹⁵³ Sasa, Baba, ninaomba ya kwamba, wakati tumekusanyika pamoja, katika dakika chache zijazo, kwamba Wewe utafanya mambo haya haya miongoni mwetu usiku wa leo, uliyofanya miaka elfu mbili iliyopita, kabla ya kusulubiwa Kwako, ulipokuwa duniani, ndipo tutajua ya kwamba Wewe ni yeye yule jana, leo, na hata milele, na kujua ya kwamba hakuna nguvu, hakuna wakati, hakuna kipindi, hakuna kitu kinachoweza kumwua Kristo wetu aliyefufuka. Yeye yu hai milele, na ana funguo za mauti na kuzimu, naye huyamwaga maji ya Uzima bure, kwa kuwa yeyote atakaye na aje anywe. Tujalie, Baba.

¹⁵⁴ Samehe dhambi zetu sasa, na utufunge ubavuni Mwako, tuseme, utufunike kwa Uwepo Wako, na utupe mambo haya ambayo tumezungumzia usiku wa leo, katika uthibitisho wa Neno Lako Mwenyewe. Katika Jina la Yesu Kristo, tunaomba kwa ajili ya utukufu wa Mungu, na kulijenga Kanisa Lake, na wale wanaokaa karibu na mji huu. Katika Jina la Yesu tunaomba. Amina.

¹⁵⁵ Sasa, tafadhali... (Billy, ulisambaza kadi chache?) Sasa, kila siku... Nadhani wao... Ndugu Borders ametuelezea kile tulicho nacho... jinsi tufanyavyo. Tunashuka kila siku na kusambaza kadi za maombi kama mnazihitaji. Huyu mvulana anakuja hapa mbele yenu, anazichanganya kadi hizi za maombi na kuzisambaza kwa mtu yeyote anayezitaka. Halafu basi kutoka hapo, hakuna mtu anayejua mahali tutakapoitia, maana mikutano midogo kama hii, labda isingeleta tofauti yoyote.

¹⁵⁶ Lakini unapokuwa na mikutano mikubwa, hivi kwamba wanasongamana na kusukumana, na kadhalika namna hii, hatutaki jambo hilo. Si ninii... ingawa panaonekana kama uwanja wa michezo, bali sasa pamewekwa wakfu kwa ajili ya Ufalme wa Mungu, ni kanisa. Nasi tuko—tuko hapa kuwa na uchaji na utaratibu. Nasi tunakutazamia Kuja kwa Bwana Yesu na Uwepo Wake miongoni mwetu, nasi hatuna budi kuwa na kicho.

¹⁵⁷ Sasa, simaanishi kutokumsifu Bwana, ninaamini, loo, jamani, “Wakinyamazaza, miamba itapiga kelele mara moja,” mnaona. Wao... Ninaamini katika kumwabudu Bwana. Lakini hatuna budi kuja mbele Zake kwa uchaji na katika uwe... katika Uwepo Wake.

¹⁵⁸ Sasa, ninaamini... Ilikuwa ni moja hadi mia moja ama...? Hakuninii... alisema hapakuwapo na wengi sana hapa wa

kusambaziwa kadi, kwa hiyo tuziite tu kadi zetu kwa dakika moja, halafu sisi...kwa kuwa wana kadi za maombi, nasi tuzimalizie, na ndipo tunaweza...

¹⁵⁹ Mambo haya hayaji tu mikutanoni hivi. Kuna baadhi ya watu wanaoketi hapa wanaoambatana nami mikutanoni. Loo, jamani! Huko nyumbani inaelezea maelfu na makumi ya maelfu ya mambo, hakuna hata wakati mmoja imewahi kushindwa, haitashindwa kamwe, haiwezi. Mradi tu ni Mungu, haiwezi kushindwa.

¹⁶⁰ Hebu tuite...Ni nani aliye na kadi ya maombi namba moja? Angalieni mahali ilipo. Wanaweza...Kadi ya maombi namba moja? Namba mbili, kadi ya maombi namba mbili? Sasa, huenda ikawa ni kiziwi, mtu fulani anayezungumza Kihispaniola. Ni nani anayeweza kuzungumza Kihispaniola? Mbili? Vema. Moja, mbili, njoni papa hapa, hebu tupange tu mstari mdogo hapa, kwa dakika chache tu, tufanye tu mstari mdogo wa maombi. Moja, mbili. Inua mkono wako ninapoita namba yako. Mbili, tatu. Ni nani aliye na tatu, kadi ya maombi namba tatu? Hapa? Njoo papa hapa.

¹⁶¹ Kama huwezi kusimama sasa, tutakubeba. Namba tatu. Namba nne, ni nani aliye na nne? Moja, mbili, tatu, nne. Moja, mbili, tatu, nne. Vema. Tano, ni nani aliye na tano? Vema, Bwana. Namba sita, namba saba, namba saba. Si—sikuiona, samahani. Namba saba, wapi? Papo hapo.

¹⁶² Sasa, sikilizeni kwa makini sana sasa, kusudi sisi... Mnaona, wakati mwingine wanapoondoka mkutanoni, wanasema, “Ndugu Branham, mimi—mimi,” ananiandikia barua, anasema, “Nilikuwa kiziwi, hakuna mtu aliyeniambia. Namba yangu iliitwa, wala sikuja hapo juu.”

¹⁶³ Haikubidi kupanda hapa juu, inakubidi kuwa na imani. Lakini wakati mwingine mtu amefanya jambo fulani maishani mwao ambalo limesababisha...Sasa, kama unaogopa dhambi kutajwa, afadhali ukae nje ya mstari wa maombi, unaona.

¹⁶⁴ Sasa, sasa, saba, nane, tisa. Nane, ni nani aliye na nane, kadi ya maombi nane? Vema, mama huyu hapa. Tisa, ni nani aliye na tisa? Kadi ya maombi namba tisa? Ungesemaje katika Kihispaniola? [Mtu fulani anasema, “Nueve.”—Mh.] Nueve. Tisa, kumi. Labda mtu fulani aliichukua akaenda nyumbani. Kumi. La. Ulikuwa na kumi, Mama? Kumi na moja, kumi na moja.

¹⁶⁵ Aisee, sikiliza, rafiki, unapokuja kuchukua kadi, usichukue kadi isipokuwa utaitumia. Hebu mtu mwingine aichukue anayehitaji, mnaona, kuingia kwenye mstari wa maombi. Hebu tuachie hapo kwa dakika moja. Tuwaombe, hawa tu hapa.

¹⁶⁶ Sasa, ni wangapi hapa ndani wasio na kadi ya maombi, nawe unataka Mungu akuponye? Inua tu mkono wako. Vema. Inaonekana kana kwamba ni karibu kila mahali, huko nyuma.

¹⁶⁷ Sasa, angalieni, kulikuwako na maskini mwanamke mmoja wakati mmoja, hakuwa, tuseme hakuwa na kadi ya maombi, bali alimwamini Yeye, naye akasema, “Kama nikiweza tu kugusa upindo wa vazi Lake, nitapona.” Hiyo ni kweli? Vema, sasa, naye akamgusa.

Sasa, kumbukeni, Yeye hakujuu shida yake ilikuwa ni nini, bali alisema, “Ni nani aliyenigusa? Ni nani aliyenigusa?”

Ndipo Petro akamkemea, akasema, “Ati ni nani aliyenigusa?” Vema, kila mtu anakugusa Wewe.”

¹⁶⁸ Akasema, “Lakini naona kwamba nguvu...” Huo ni uweza. “Nimekuwa dhaifu.” Akasema, “Nguvu zimenitoka. Ni nani aliyenigusa?” Ndipo hatimaye akaangalia kote kwenye kusanyiko mpaka akamwona maskini mwanamke yule aliyemgusa. Huenda alisimama huko nyuma kabisa ama hapa. Naye akamwambia kuhusu kutokwa kwake na damu na kusema imani yake ilikuwa imemwoko. Ni wangapi wanaojua hadithi hiyo? Vema. Sasa, sikilizeni kwa makini sasa. Liwekeni katika Maandiko.

¹⁶⁹ Kama ni yeye yule jana, leo, na hata milele, basi Biblia inasema, hawa makasisi, wachungaji wenu hapa, watasoma, hivi Biblia haise mi Yeye ni Kuhani Mkuu, sasa hivi, anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu? Hiyo ni kweli? Basi angetendaje? Kama Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule, angetenda vivyo hivyo. Hiyo ni kweli? Sasa, ni wangapi wanaoamini hilo? Angetenda vivyo hivyo. Ndipo unamgusa kwa mambo ya udhaifu wako.

¹⁷⁰ Useme, “Mimi... Bwana, ninakuamini Wewe, nami ninataka Wewe u—uniponye. Nami ninajua mtu huyo aliyesimama pale hanihui, bali hebu niguse vazi Lako. Baba Mungu, unirehemu. Sasa, yeye aliniambia ya kwamba Wewe ulikuwa yeye yule, na Wewe ndiwe Roho aliye hapa, Yule ambaye hatumwoni. Lakini ninaamini ya kwamba mimi ni mwaminio, nami ninakupenda, na hebu niguse vazi Lako, ndipo Wewe ujibu kupitia ndugu yetu, kama ulivyofanya kupitia Mwanao, na—na halafu mimi—mimi... ita—itanithibitishia kwamba Wewe ni Bwana Yesu yeye yule.”

Sasa hivi hilo si lingekuwa zuri kama Yeye angefanya hivyo? Sasa, wewe liamini, uone kama Yeye hatalifanya. Wewe liamini tu.

¹⁷¹ Sasa, mtu wa kwanza anayekuja, huyu ni mwanamume, sasa, mwanamume, labda mdogo wa umri kuliko mimi. Simjui, sijawahi kukuona maishani mwangu, ni mwanamume tu. Nami nadhani hatufahamiani. Na sasa, kusudi kusanyiko lijue ya kwamba hatufahamiani, mmoja kwa mwingine, kusudi tu tushikilie ninii yetu... inua tu mkono wako kusudi, waone kwamba hatufahamiani.

¹⁷² Sasa, sijawahi kumwona nijuavyo mimi. Huenda aliniona mahali fulani mikutanoni. Kama amekuwa katika mikutano mingine, ama kitu fulani, huenda aliniona, lakini kusema kumjua, simjui. Sijui lolote kumhusu, bali Mungu anamjua, mnaona.

¹⁷³ Sasa, hawa hapa watu wawili wakikutana kwa mara ya kwanza maishani. Na sasa, kama mtu huyo alikuwa ni mgonjwa, na chochote ningaliweza kufanya kumsaidia, hakika ni—ningefanya hivyo, Ninge—ningemsaidia, ningefanya yote niwezayo kumsaidia.

¹⁷⁴ Na kama ningeweza kumponya, bila shaka ningefanya hivyo upesi sana, bali uponyaji hauko ndani yangu, uponyaji ni jambo ambalo tayari limefanywa, “kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa.” Kila dhambi ilisamehewa wakati Yesu alipokufa msalabani, kila mwenye dhambi alisamehewa papo...kama sivyo, Mungu angeuangamiza ulimwengu wote sasa.

¹⁷⁵ Ni Damu ya Yesu Kristo, kama bamba, inayoshikilia ulimwengu kutoka...pamoja sasa hivi. Lakini siku moja Damu hiyo itaondolewa, halafu basi, kama ukifa katika dhambi zako na hukubali msamaha huo, unasimama mbele za Mungu mwenye dhambi. Unaona? Lakini kuhusu dhambi zako, tayari zimesamehewa, bali inakubidi kukubali msamaha huo. Nao uponyaji tayari umefanywa, “kwa kupigwa Kwake,” Petro alisema, “*tuliponywa*” wakati uliopita, “*tuliponywa*.” Sasa, huna budi kuukubali uponyaji wako.

¹⁷⁶ Sasa, mchungaji wenu anawaambia habari zake, Ndugu Roberts huja na kuomba, na kuwawekea watu mikono, na kadhalika namna hiyo, hilo ni thibitisho. Sasa, tuseme, kwa mtu huyu hapa, kama ningesema, “Bwana, shida yako ni nini?” Labda angeniambia, na labda yeye hayuko kwa ajili yake mwenyewe, labda anasimama kwa ajili ya mtu mwingine. Labda yeye—labda ana matatizo ya kifedha, labda ni shida za kinyumbani, labda amefanya jambo fulani maishani linalomzuia, sijui, yeye amesimama tu hapo, yeye ni mwanamume.

¹⁷⁷ Lakini Roho Mtakatifu anajua yote kulihusu. Kama Roho Mtakatifu anaweza kumwambia kile kilichokuwako, atajua kama hiyo ni kweli ama si kweli, hakika, kama Yeye angemwambia yatakayotukia (Kama angeweza kumwambia yale ambayo yamekuwako, yeye ajua kama ni kweli ama si kweli.), basi angejua ahadi Yake itakuwa nini, itakuwa hivyo, haina budi kuwa hivyo. Unaamini hilo? Vema, Bwana. Sasa, Bwana na akujalie haja yako.

¹⁷⁸ “Yesu yeye yule jana, leo, na hata milele.” “Mabwana, Sisi Tunataka Kumwona Yesu.” Bwana wetu mpendwa, aliye hapa katika umbo la Roho Mtakatifu, tukitumainia Yeye yuko juu ya mtu huyu, juu yangu, na kwa imani yako mwenyewe

katika karama ya Kiungu iliyotumwa kutoka kwa Mungu inatimiza hiyo haja, ninatumaini ya kwamba itatimiza. Bila kukujua, bila kujua chochote kukuhusu, hatufahamiani kabisa, na kama Bwana ataniambia kilichokuleta hapa, ama jambo fulani kukuhusu wewe...

¹⁷⁹ Sasa, mnasema, “Kile yeye...?” Mtu fulani huko nje anasema, “Anafanya nini sasa?” Jinsi hasa Yesu alivyomfanyia yule mwanamke kisimani. Baba alinituma Santa Maria. Sasa nipo hapa, sijui ni kwa sababu gani, lakini huyu hapa mtu wa kwanza anayekuja mbele yangu, kwa hiyo ninazungumza naye kama alivyomzungumzia yule mwanamke kisimani, ni kuwasiliana na roho yake.

Unasema, “Sasa, hiyo ni nini?” Sasa, ngoja kidogo tu. Hebu na tulinyoshe hili sasa, nilihisi kitu fulani kikiingia kutoka huko nje. Mnaona?

¹⁸⁰ Angalieni, “Hapo mwanzo kulikuwako Neno, huyo Neno alikuwa kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu.” Hiyo ni kweli? Waebrania 4 ilisema, “Neno la Mungu ni kali, lina nguvu kuliko upanga ukatao kuwili, likichoma mafuta yaliyomo ndani ya mfupa, na Mtambuzi wa mawazo na makusudi ya moyo.” Hiyo ni kweli? Neno la Mungu! “Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu ndani yenu...” Mnaona ninalomaanisha? Ni Neno lililofanyika mwili miongoni mwenye. Mnaona? Neno! Na Neno hilo lililokuwa huko nyuma, ambalo haliweze kubadilika, ni Neno lile lile usiku wa leo, ambalo lingemtangaza Masihi yeye yule, si mimi, bali Yeye, Masihi yeye yule. Ninaamini mtu huyu anaamini hilo.

¹⁸¹ Nitasimama karibu kidogo na maikrofoni kwa sababu, wakati mwingine maono yanapokuja, ninii... Sijui ninalosema, ni mahali pengine tu, mnaona. Mnaweza kunisikia vizuri, kila mtu? Sasa, sijui kama Yeye atamwambia au la, lakini ninaamini atamwambia. Sasa, kama ningekuwa na nguvu za kukuponya, ningefanya hivyo, bali ninakutangazia tu ya kwamba tayari umeponywa, kama unahitaji uponyaji ama chochote kilicho shida.

¹⁸² Lakini, unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Sasa, hilo ndilo aliloniuliza, yule Malaika ambaye, anayeonekana katika ile picha ya ile Nguzo ya Moto. Wanayo hapa sasa. Mnaona? Unaiona ile picha? Umeiona kwenye ile picha? Hiyo imekaa moja kwa moja kati yangu na wewe sasa hivi. Una shida ya tumbo, ulifanyiwa upasuaji. Hiyo ni kweli, sivyo? Unaamini?

¹⁸³ Sasa, “Tunataka kumwona Yesu.” Sasa, siwezi kuwaambia sasa hivi yale Yeye aliyosema, Huyu hakuwa ni mimi. Sijui lolote kumhusu mtu huyo, chochote kile, nitakipata kwenye kinasu sauti. Sijui kamwe nilichomwambia, ilikuwa ni mahali pengine. Niliona jambo fulani likitukia, bali ni—nisingeweza kuwaambia sasa kile lilichokuwa. Unaona? Huyu alikuwa ni Yeye.

¹⁸⁴ Ni kwa nini, mara ya kwanza, ile mikutano, daima unakuta kwamba mtu fulani, alisema, “Alibahatisha hilo”? Sikubahatisha hilo. Hubahatishi mambo kama hayo kikamilifu mara mamilion. Hapa, kama mnafikiri ilikuwa ni kubahatisha, hebu kidogo.

¹⁸⁵ Niangalie tena, Bwana. Hebu nione kwa muda kidogo tu. Naam, Bwana. Ugonjwa wa tumbo, upasuaji. Hiyo ni—hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Hutoki hapa, unatoka Bakersfield. Hiyo ni kweli. Huyu ni mke wako aliyeketi hapo, yeye ni mgonjwa pia, anataka kuombewa. Unaamini Mungu anaweza kuniambia shida yake ni ipi? Ugonjwa wa kibofu. Hiyo ni kweli? Inua mkono wako kama hiyo ni kweli. Vema. Bw. Ackley, mnaweza kurudi nyumbani, nyote mnapata afya. Yesu Kristo anawaponya. Amini kwa moyo wako wote. Mungu awabariki.

¹⁸⁶ Unasema, “Ulijuaje jina lake?” Vema, ni Masihi yeye yule. Hivi hamwezi kuona? Si mimi, Yeye. Mtaamini sasa? Sasa, mkitaka kusema, “Bwana asifiwe,” mnaweza kusema, mnaona. “Bwana asifiwe.” Mnaona? Sasa, Mungu ni kitu cha kuabudiwa. Hatuna budi kuamini kwa moyo wetu wote.

¹⁸⁷ U hali gani, Mama? Hatufahamiani, sikujui hata kidogo, bali Mungu anakujua. Unaamini kama Mungu anaweza kuniambia shida yako ama kitu fulani moyoni mwako, unaamini ya kwamba utakuwa mzima? Unaamini? Tuko makini, Mama, umetiwa uvuli wa mauti, unaona, kivuli cheusi: ulikuwa na kansa, upasuaji, tumbo, hali mbaya sana. Hiyo ni kweli. Lakini kama utamwamini Mungu kwa moyo wako wote, hiyo ndiyo nafasi pekee, kitu pekee ambapo huna budi kuwa mzima.

¹⁸⁸ Kulikuwa na wenye ukoma walioketi langoni usiku mmoja, nao wakasema, “Tukiingia ndani, ni mauti mle ndani, kwa sababu wanakula watoto wenyewe kwa wenyewe.” Washami waliwazingira. “Tukiketi hapa tutakufa, lakini tukishuka kwenda kwenye kambi ya adui, basi wanaweza kutuokoa.” Mnaona?

¹⁸⁹ Lakini ninaona kivuli hicho cheusi juu yako. Sasa, huombwi kushuka kwenda kwenye kambi ya adui, unaombwa na kutarajiwa kwenye Ki—Kiti cha Enzi cha Baba mwenye upendo. Utamwamini? Njoo hapa kwa muda kidogo tu. Hebu niushike mkono wako.

¹⁹⁰ Baba wa Mbinguni, wakati Roho Mtakatifu akiwa hapa, uovu huu unaomwua mwanamke huyu, hawezi kuishi ila kidogo tu, jalia nguvu za Mwenyezi Mungu zimlaani adui huyu, na jalia aishi. Kwa ajili ya Ufalme wa Mungu, ninaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Mungu akubariki. Usiwe na shaka sasa, nenda ukiamini.

Sasa, lazima tu uwe na imani ya kuamini, “Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana.”

¹⁹¹ U hali gani? Unaamini kwa moyo wako wote? Sasa, unajua sikujui, hatufahamiani, lakini Mungu anakujua. Huko hapa kwa ajili yako mwenyewe, uko hapa kwa ajili ya mtu mwingine, watu wawili. Mmoja wao yuko hapa California, huyo mwingine yuko Arkansas. Amini kwa moyo wako wote. Mmoja akiwa na ugonjwa wa jicho, na huyo mwingine akiwa na shida ya kinena. Amini kwa moyo wako wote, na wote wawili watapata afya. Nenda ukiamini. Amina. Hiyo ni kweli. Mungu akubariki. Amini.

Unaamini? Kamwe usiwe na shaka.

¹⁹² Ilikugusa, sivyo, Dada? hasa niliposema kansa. Usiogope, ulimgusa Yeye. Alimgusa nani? Maskini mama huyo anaugua, hapo, akiwa na ugonjwa wa kansa ya ngozi, inamrudia wakati wote. Hiyo ni kweli, inua mikono yako. Wewe amini. Mungu awabariki. Kitu hicho na kilaaniwe! Kama una imani ya kutosha kugusa upindo wa vazi Lake, kusudi ajibu kupitia kwangu na kuniambia kile ulichokuwa ukizungumzia, basi amini.

¹⁹³ Unaamini? Mwamini Mungu. “Mabwana, Sisi Tunataka Kumwona Yesu.” Huyu Ndiye, Yule mpendwa aliyekuokoa. Huyu hapa papa hapa, katika siku za mwisho, kabla tu Kanisa halijachukuliwa, papa hapa akijithibitisha Yeye yule jana, leo, na hata milele. Wazieni tu, yale aliyofanya tayari, yale aliyofanya tayari yamekusanywa pamoja kuliko yale aliyofanya tangu huko nyuma kabisa katika Kanisa la mwanzoni. Wazieni hilo! Ndivyo hasa Maandiko yalivyoahidi, maana asingeweza kulifanya mpaka wakati huu. Sasa, waangalieni tu watu sasa. Iweni na kicho kabisa. Popote mlipo, ombeni, mwaminini Mungu. Mungu atawajalia.

Unaamini Mungu, atakuponya ugonjwa huo wa mguu? Una tatizo kwenye mguu wako. Amini kwa moyo wako wote.

Sasa, aligusa nini? Mnaona? Alimgusa Yeye. Mnaona? Hilo hapo. Mnaona?

¹⁹⁴ Kamwe usiwe na shaka, utapona. Sasa, huna budi kubaki na imani ile ile uliyo nayo sasa. Kama kamwe ukipoteza imani yako, litarudi. Endelea tu kuamini, hivyo tu. Dumu na imani iyo hiyo. Petro alitembea maadamu aliamini, lakini alipoanza kushuku, akaanza kuzama. Usi—usifanye hivyo sasa, una imani ya kutosha kwa ajili ya jambo hilo.

¹⁹⁵ Je, umeshawishika ya kwamba Yesu Kristo yuko pamoja nasi? Hapa ama huko nje, si lazima mwe na kadi za maombi, inawabidi tu kuwa na imani. Yeye si ni Masihi yeye yule?

¹⁹⁶ Tuna mama mwingine hapa jukwaani. Hebu na tuzungumze naye kidogo. Sasa, unatambua ya kwamba kila kitu kinazunguka-zunguka, kunizunguka sasa. Unaona? Kama mtu mmoja kugusa upindo wa vazi Lake kulimfanya Mwana wa Mungu kuwa dhaifu, na mimi je, mwenye dhambi aliyekolewa kwa neema? Unaona? Unaona? Danieli aliona ono moja,

likamsumbua kichwani kwa siku nyingi. Sasa, unaweza kuwazia kile inachokufanyia.

¹⁹⁷ Inajaribu nini. . . anajaribu kufanya nini? Kuwafanya ninyi nyote kumwamini Yeye. Yeye yupo hapa, Uwepo Wake upo hapa. Haileti tofauti yoyote kilicho shida yako, mwamini Yeye. Usitilie shaka, iweni tu na imani.

¹⁹⁸ Angalieni hapa, Dada. Kutokana na mtetemo wa roho unaotoka kwako, wewe ni mwaminio. Jambo ndilo hilo, unaamini. Mimi ni mwaminio. Nasi tunasimama hapa kwa mara ze—zetu za kwanza nadhani, za kukutana maishani, nijuavyo mimi. Huenda umeniona mahali fulani mikutanoni, ama kitu fulani. Au hivi hii ndiyo mara ya kwanza tumewahi kukutana? [Mwanamke huyo anasema, “La.”—Mh.] Wewe. . . Tulikutana hapo awali? [“Naam, Bwana.”] Lakini sikujui. [“La.”] La, sikujui. Vema. Bila shaka, kuna watu wengi sana wanaohudhuria mikutano mahali mbalimbali, nisingejua.

Lakini kama Bwana anaweza kuniambia kilichokuleta hapa ama jambo fulani kukuhusu, lingekuwa la kushawishi sana kwamba Yeye, Yeye anajua yote kulihusu, sivyo?

¹⁹⁹ Ingekuwa kwenu nyote? Mnaona? Anaonekana kama mtu mzuri, na hata hivyo anaweza kuwa ni mdanganyifu amesimama hapo. Kama ndivyo, angalieni tu kitakachotukia. Tumewafanya wafanye hivyo.

²⁰⁰ La, mama ni mgonjwa. Ana ugonjwa wa tumbo pia, ni vidonda, wasiwasi sana, matatizo, ninii tu. . . Hiyo ni kweli. Mahututi sana, sana. Unaamini Yeye atakuponya? Je, mambo hayo ni kweli, yale yaliyosemwa sasa hivi? Inua mkono wako kama hiyo ni kweli. Sasa, unaamini?

²⁰¹ Yeye ni mtu mzuri sana, ninaamini nitazungumza naye kidogo tu zaidi, bila shaka, kadiri unavyozungumza, ndivyo inavyosema mengi, ndivyo unavyozidi kuwa dhaifu. Kwa kuwa yeye ni. . . anaonekana kuwa na nia njema. . . [Dada huyo anaitika—Mh.] Na—najua unaamini, Dada. Mama yako ni mgonjwa pia. Unaamini Yeye anaweza kuniambia mama yako ana shida gani? Ni kutokwa na damu matumboni. Hiyo ni kweli. Uh-huh. Baba yako, hospitalini, upasuaji wa kibofu. Naye mume wako pale, ana mishipa iliyovimba miguuni mwake, yeye. . . Sasa, wewe amini tu na uende zako. Vema, Mungu akubariki.

²⁰² Njoo ukiamini kwa moyo wako wote sasa. Vema, Bwana. Njoo. Unaamini Mungu anaweza kukuponya huo ugonjwa wa mgongo, akupe afya? Endelea tu kupitia jukwaani, useme, “Asante, Bwana Yesu, mimi. . .” Vema, Bwana.

²⁰³ Mwambie tu arudi upande huu mwingine, Paulo, ama aje huku, ukitaka. Unajua, Bwana, Yeye anaweza kuponya ugonjwa wa moyo kama vile anavyoweza kuponya kitu kingine chochote. Unaamini hilo? Vema, Bwana. Toka tu jukwaani,

useme, “Asante, Bwana, kwa kuniponya na kunipa afya.” Uh-huh. Uh-huh.

204 Sasa, wewe, bila shaka, mtu yeyote anamwona akiwa mgumu namna hiyo. Je, utaamini upako wa Roho Mtakatifu, kama nikikuwekea tu mikono, utapata afya? Unaami-. . .? Njoo hapa kwa dakika moja. Baba yetu wa Mbinguni, katika Jina la Yesu Kristo ninaomba kwamba umpe afya. Amina. Sasa, usitilie shaka. Nenda ukiamini sasa na uwe na imani.

205 Njoo. Hilo ni sawa, Mama, songa mbele moja kwa moja. Vema. Una wasiwasi, una ugonjwa wa moyo, unadunda upesi, kila kitu, hasa baada ya kula na kujilaza chini. Kwa kweli si moyo wako, ni ugonjwa wa wasiwasi. Kama wewe. . . una moyo wenye wasiwasi, sasa, kama ukiamini kwa moyo wako wote, kitu hicho kitakoma, hakitakusumbua tena. Unaamini hilo? Basi ondoka kwenye hiyo safu ukisema, “Asante, Mungu mpenzi,” na upate afya.

206 Ni ugonjwa wa damu, upungufu wa damu. Lakini, unaamini ya kwamba Mungu anaweza kukupa damu, usiku wa leo, kutoka Kalvari? Unaikubali? Nenda, ukiamini kwa moyo wako wote na Mungu. . .? . . .

207 Unaamini? Kila mtu hapa ndani unaamini kwa moyo wako wote? “Mabwana, Sisi Tunataka Kumwona Yesu.” Je, mnatambua, enyi marafiki, ya kwamba Huo ni Uwepo Wake hapa? Je, mnautambua? Mnaijua hiyo hisi tamu, tamu sana, nyenyekevu? Sasa, ni wangapi wenu mlio waaminio, tena sasa, na mnaliamini kwa moyo wenu wote?

208 Sasa, ninataka kuwaambia yale Biblia isemayo hapa. Katika agizo la mwisho Yesu alilolipa Kanisa Lake, Yeye alisema, “Ishara hizi. . .” (Niliona jambo lingine likitukia huko nyuma. Ugonjwa huo wa figo, ulikuacha, sahau tu jambo hilo.) “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Wakati Roho Mtakatifu yupo sasa, nawe unataka kuponywa, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Hiyo ni kweli? Sasa, wewe weka mikono yako juu ya mtu aliyeketi karibu nawe. Weka tu mikono yako juu ya mtu aliyeketi karibu nawe. Sasa, usijiombee, wewe waombee, maana wanakuombea. Unaona? Na hebu tuombe sasa ya kwamba Mungu atamponya kila mtu mahali hapa.

209 Baba yetu wa Mbinguni, ninatoa maombi yangu kwa ajili ya hawa walio hapa, usiku wa leo, walio wahitaji. Wamewekeana mikono. Wewe upo daima kuponya. Tusingeweza kukushuku, Bwana, tena, Wewe upo hapa. Tunajua ya kwamba hao watu wasingeweza kufanya hivyo, wala mimi nisingeweza kufanya hivyo. Sote tunajua ya kwamba ni Mungu miongoni mwetu, Mungu Baba mkuu katika umbo la Roho Mtakatifu. Yehova mkuu yuko miongoni mwetu.

²¹⁰ Alisema, alipokuwa hapa katika umbo la Bwana Yesu, Yeye alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya. Kule kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa yule, na Mungu atamwinua; kama wamefanya dhambi, watasamehewa.”

²¹¹ Ee Mungu wa Mbinguni, tusamehe kutokuamini kwetu. Tunajua hiyo ndiyo dhambi pekee iliyopo, dhambi ya kutokuamini. Na jalia Roho Mtakatifu aje *sana* juu ya kila mtu, sasa hivi, hata hawatakosa kuamini tena, kwa sababu ya Uwepo wa Kristo, usiku wa leo, akijionyesha Mwenyewe kuwa hai baada ya miaka elfu mbili, Neno Mwenyewe akisimama hapa miongoni mweni, ndani yetu, akilidhihirisha Neno Lake.

²¹² Shetani, wewe ambaye umewachefua watu hawa, ukajeruhi miili yao, ukawatesa, wewe ni kiumbe kilichoshindwa. Bwana wetu Yesu Kristo alikushinda pale Kalvari. Umeshindwa. Huna nguvu hata kidogo. Nasi tunakuja tukiamini, huku imani yetu imefunguliwa mbele za Mungu. Achana na kila mmoja wao. Katika Jina la Yesu Kristo, toka kwenye kusanyiko hili. Na jalia waende nyumbani na wawe huru na magonjwa yote na mateso.

²¹³ Sasa, huku vichwa vyetu vimeinamishwa mnapoendelea kuomba, kuna mwenye dhambi, mwanamume au mwanamke, mvulana au msichana, hapa usiyemjua Kristo kama Mwokozi wako, nawe unaamini kwamba tendo hili la Roho Mtakatifu ni kulingana na Neno la Mungu, nawe unataka kuokolewa? Waweza kutembea hapa karibu na maskini madhabahu hii, usiku wa leo, na uache nikupe mkono na kuomba pamoja nawe? Waweza kuja huku sasa hivi? Inuka tu kutoka kwenye kiti chako.

²¹⁴ Mimi siko sana katika kushawishi. Kama Roho Mtakatifu hawezi kushawishi kwa kazi Zake, basi hakuna haja ya mimi kushawishi. Lakini kama wewe, kama unajua kwamba huko vizuri na Mungu, nawe ungetaka tukuombe, tuko hapa kufanya hivyo. Sisi ndio mtumishi wa umma wa Bwana Yesu Kristo, mimi na wahudumu hawa hapa pamoja tuko hapa kukusaidia, kukuelekeza jinsi ya kumpata Yesu kama Mwokozi wako.

²¹⁵ Kama ungetaka kuja, njoo huku sasa, wakati tukivumisha tu wimbo huo anaoucheza pale, *Karibu Nimeshawishika*, kama ungetupa sauti ya huo, Ndugu. Na wakati kila Mkristo, katika maombi sasa, na kwa kuwa Uwepo wa Roho Mtakatifu... Kusudi lake kuu ni kumwokoa mtu fulani, kumfanya mtu fulani aokolewe. Sasa, wakati tumeinamisha vichwa vyetu, kila mtu akimwomba mwenzake:

“Karibu nimeshawishika” sasa kuamini;

“Karibu nimeshawishika” Kristo kumpokea;

Inaonekana sasa...

²¹⁶ Hivi hutakuja wakati tunapongojea sasa? Sasa, kama huko chini ya Damu ya Kristo, ungewezaje kusimama na kuona kazi ya Mungu ikisimuliwa kutoka kwenye Biblia, akidhihirishwa

hapa miongoni mwetu, na kisha uondoke bila kumjua Yeye? Hivi hutakuja? Tunakualika sasa.

Mara moja tu zaidi, tunapouvumisha. Sisi sote pamoja. [Ndugu Branham anavumisha—Mh.]

Sasa, kwani unafikiri Yeye hajui unachowazia? Bila shaka. Ninaweza kukiona paa hapa.

²¹⁷ Usitilie shaka tena, njoo. Kwa nini uishi kwa njia ya kufadhaika? Njoo, uwe na hakika, maana huenda ikawa imechelewa sana kesho, huenda hii ikawa ndiyo siku yako ya mwisho duniani. Amini sasa na uje, hivi hutakuja?

Sasa, huku vichwa vyetu vimeinamishwa tena:

Karibu. . .

²¹⁸ Kila mtu akiomba, kila Mkristo sasa. Mungu awabariki. Ninaomba pamoja nanyi, na kuomba ya kwamba Mungu atakuokoa, akuponye na kukupa afya, akupe afya na nguvu.

Inaonekana sasa mtu fulani aseme, Nenda,
Roho, nenda Zako;

Ungewezaje kupata siku *inayofaa* zaidi, inayofaa kuliko hii ilivyo, Uwepo Wake ukiwa hapa, Yule anayejua hata kile unachowazia?

. . . nitakuita Wewe.

²¹⁹ Baba yetu wa Mbinguni, kwa ajili ya Uwepo Wako tunashukuru. Katika uwanja huu mdogo hapa, usiku wa leo, ambapo mpira wa vikapu, labda, unachezwa, na mazoezi ya jeshi, Wewe pia unawazoeza na kuwafunza askari usiku wa leo, Bwana, wa lile jeshi kuu la wokovu la Mungu, ukiwapa mazoezi katika imani wapate kuamini, watoke hapa kama waokoaji halisi wa nafsi, watakoachukua simu, na kuwapigia simu majirani, na kuwaleta watu ndani, kuwaingiza ndani, wale ambao si Wakristo, wale walio wagonjwa na wanaoteseka.

²²⁰ Baba, ninaomba ya kwamba kila mtu anayeingia kwenye chumba hiki ambaye ni mgonjwa au anayeteseka ataponywa, na kila mwenye dhambi apitaye katika milango hii hatakuwa na amani hata watakapokuja Kwako, kwamba kila mwaminio anayeingia katika milango hii atabatizwa kwa Roho Mtakatifu, na ishara kuu na maajabu yanaweza kufanywa, Bwana. Tunakushukuru, Bwana.

²²¹ Baada ya miaka elfu mbili tunaona thibitisho lisiloweza kukosea ya kwamba tungali tunaweza kumwona Yesu, Yeye anaonekana miongoni mwetu kabla tu ya kuja Kwake. Yeye anaonekana katika Kanisa Lake, ishara ya mwisho aliyofanya mbele ya Wayahudi, Naye akamalizana nao, ishara ya mwisho ambayo ametoa kabla ya Mataifa kumalizika, inaonyeshwa. Tunajua hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya mwisho ambayo Ibrahimu aliona kabla ya Sodoma kuteketezwa, ndiyo ishara ya mwisho.

222 Tunatambua ya kwamba wahudumu wako huko nje Sodoma, usiku wa leo, miamsho mikubwa inaendelea kupitia Chicago na kote ulimwenguni, ishara kuu na maajabu yanatendeka, wahudumu wakihubiri, wakilia kwa mioyo yao yote, wachungaji wakiomba na kusihi, maajabu makuu yakifanywa na Roho Mtakatifu kote ulimwenguni: uponyaji, ishara, maajabu.

223 Mungu, kamwe huyatumi mambo haya... Kamwe huleti Hukumu kabla hujatuma onyo kwanza, nasi tunaona ya kwamba ishara ya onyo imeshuka, taa nyekundu inamulika. Ee Mungu, jalia wanaume na wanawake wahusike wao kwa wao, jalia washughulikie kizazi hiki kiovu cha watu wanaoangamia, wakiondoka hapa bila kumjua Mungu, watakufa katika dhambi. Na, loo, jinsi... litakuwa ni jambo la kuchukiza jinsi gani siku hiyo, watakaposikia kulia na kuomboleza! Kamwe hakutakuwa na fursa nyingine wata kayopata kuona.

224 Baba, kama Rais akija kwenye mji huu usiku wa leo, bendera zingeinuliwa, maua yangetandazwa kote mitaani, na—na kungekuwa na sherehe kubwa mno. Lakini Bwana, unakuja mjini katika umbo la Roho Mtakatifu, na, Ee Mungu, inakubidi kutafuta, na kuvuta, na kusihi, na kuwashawishi watu wajitayarisha kwenda Mbinguni. Ni siku ya jinsi gani tunayoishi, Bwana!

225 Tunaomba sasa ya kwamba rehema Zako kuu zitaendelea pamoja nasi. Wabariki wahudumu hawa na makanisa yao. Ee Mungu, washa uamsho wa mtindo wa kale katika kila mmoja wao, Bwana, mpaka mioto ya uamsho iwake kote humu bondeni. Tujalie, Baba. Sisi ni watumishi Wako, tupokee, utusamehe uvivu wetu, uadui wetu, bali utusamehe, Bwana, uzembe wetu. Tunaomba ya kwamba utatusamehe tu, na kutusaidia tunapoendelea na safari.

226 Jalia Roho, kila usiku, aingie ndani zaidi na kwa nguvu zaidi kila usiku, ishara kubwa zaidi na miujiza mikuu zaidi ifanywe mbele zetu usiku baada ya usiku, Bwana, mpaka watu, halitazuilika kwao.

227 Nasi tunajua, Bwana, ya kwamba Wewe ulisema katika Neno Lako, “Wote alionipa Baba watakuja.” Ndipo wakati Nuru hiyo inapomulika kwenye Mbegu hiyo iliyochaguliwa tangu zamani, jambo fulani hutukia, kama maskini yule mwanamke mzinzi tuliyenena habari zake usiku wa leo. Alikuwa mgonjwa na amechoshwa na jinsi walivyokuwa wakifanya, kadiri tujuavyo sisi hakuwa mfuasi wa mahali popote, bali alikuwa ametangulia kuonekana na Mungu. Na mara alipoiona hiyo Nuru ikimulika, hata mbele ya makuhani wa siku hiyo, ambao hawakujua ilikuwa ni nini...

228 Kama yule kipofu, alipopata kuona, alisema, “Ajabu hii, ati ninyi ndio viongozi wa siku hizi, na hata hivyo hamjui atokako Mtu huyu, Naye hufanya mambo haya.”

²²⁹ Bwana, ndivyo ilivyo leo. Ninaomba ya kwamba utatuochochea, Bwana. Ee Mungu, tutikise, kwa kuwa huu ndio wakati wa kumalizia. Tujalie, Bwana. Tunayakabidhi mambo yote Kwako sasa kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Katika Jina la Yesu. Amina.

Hata tutakapokutana! hata tutakapokutana!
(Vema, Ndugu, Mchungaji.)

Hata tutakapokutana . . .

²³⁰ Sasa, wachungaji wenu hapa wataendelea na ibada kutoka hapa. Ninatumaini kuwaona kesho usiku. Njoni mapema, mchukue kadi zenu za maombi, mkapange mstari kwa ajili ya ibada kesho usiku. Ndugu, Mchungaji. 

62-0627 Sisi Tunataka Kumwona Yesu
National Guard Armory
Santa Maria, California Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org